# JENGA MAHUSIANO YAKO NA MUNGU

## ILI UWEZE KUACHA ALAMA KATIKA KIZAZI CHAKO

Heriel Michael

**TOLEO LA KWANZA**

**June,2019**

**Angalizo:**
Kitabu hiki ni mali halali ya Heriel Michael ni makosa kunakili au kutoa nakala za kitabu hiki Bila idhini ya mwandishi.

**Nunua nakala halisi ili kuinua huduma hii,**

Kwa maelezo zaidi pamoja na ushauri
Tunaweza kuwasiliana kupitia
Simu: +255 685 148 856
E-mail: herielmichael1@gmail.com
Face Book: Heriel Michael
Whatsup: +255 746 155 205

**ISBN 978-9987-749-53-9**

**Kimechapishwa na**

Truth Printing Company

0764 425 704/ 0652 383 590

geofreymakula@gmail.com

# YALIYOMO

DIBAJI. .......... 4
SHUKRANI .......... 6
UTANGULIZI .......... 6
SURA YA KWANZA .......... 13
*KWA NINI MUNGU ANATAKA MAHUSIANO MAZURI NA MWANADAMU?* .......... 13
SURA YA PILI .......... 30
*ILI MAOMBI YAJIBIWE* .......... 30
SURA YA TATU .......... 44
*UHUSIANO KATI YA KIZAZI CHAKO NA MAHUSIANO YAKO NA MUNGU* .......... 44
SURA YA NNE .......... 53
*FAHAMU MKAKATI ALIONAO MUNGU JUU YA MAISHA YAKO* .......... 53
HITIMISHO. .......... 56
VITABU REJEA. .......... 57

# DIBAJI.

**Mwandishi wa kitabu** hiki chenye jina la **JENGA MAHUSIANO YAKO NA MUNGU ILI UWEZE KUACHA ALAMAKATIKA KIZAZI CHAKO** kwa neema ya Mungu ameachilia maarifa kwa ajili ya msomaji yatakayomsaidia na kulisaidia kanisa kufahamu vizuri juu ya sababu za Mungu kuhitaji mahusiano mazuri na mwanadamu na kwa ufahamu huo utaiona sababu ya wewe kuchukua hatua ya kujenga mahusiano yako na Mungu aliye hai katika Kristo Yesu.

Utafahamu zaidi juu ya sababu zinazomfanya Mungu aone sababu ya kutuongoza yeye baada ya kuokoka kupitia Roho Mtakatifu na kupitia sababu hizo utaelewa zaidi juu ya Roho Mtakatifu katika kutenda kazi ndani yako na jinsi anavyoweza kukusaidia kuyaishi mapenzi ya Mungu wakati wote

Lakini kama jinsi ilivyo kwamba tunahitaji haja zetu mbele za Mungu ambaye ndiye ayafanyaye bora maisha yetu kwa njia ya maombi, mwandishi ameweka sababu zinazoweza kukuwesha kupokea majibu ya maombi yako. Ni kweli kwamba sio kila maombi tunayoomba yanajibiwa kumbe tunahitaji maarifa ya kutosha kutupa uelewa juu ya kujibiwa kwa maombi yetu na kupitia kitabu hiki utapata maarifa hayo yatakayobadilisha mtazamo wa maombi yako na kwa kutumia maarifa haya katika maombi utayaona mafanikio na majibu katika maombi.

Pia ndani ya kitabu hiki utaelewa mkakati alionao Mungu juu ya mwanadamu na kufahamu kwa upana zaidi mambo ya msingi ya kukusaidia kulitumikia kusudi la Mungu ukiwa duniani yanayokuwezesha kuacha alama ya kudumu kwa kizazi chako na vizazi vijavyo. Katika Biblia hakuna mtumishi aliyeacha alama kupitia utumishi wake ambaye hakujenga uhusiano mzuri na Mungu aliye hai.

**Rev Timothy Erasto Chimeledya- Chaplain USCF-CCT –UDOM**

**M.A (Theology & Contemporary issues).**

**Email: tchimmy1032@yahoo.com.uk**

**Phone: +255 762 838 115&+255 686 243 856.**

## SHUKRANI

Ninamshukuru sana mwenyenzi Mungu kwa neema yake ya ajabu maishani mwangu kwa kuniwezesha kuandika kitabu hiki. Nimeuona mkono wa wake katika kazi hii tangu aliponipa huduma ya uandishi wa vitabu.

Shukrani za kipekee ziwaendee wazazi wangu **Mr&Mrs Michael Hillonga** kwa malezi yao mazuri kiroho na kimwili. Wamekuwa mwanga katika njia zangu na kufanyika daraja kwangu katika maeneo mbalimbali. **Mungu awabariki sana na kuwapa maisha ya baraka na amani.**

Ninamshukuru Mchungaji mlezi wa **USCF-CCT-UDOM CHAPLAIN Rev Timothy Erasto Chimeledya** kwa jinsi alivyonitunza na kunikuza kiroho kwa muda wote niliokuwa chuoni. Amefanyika baraka kwenye maisha yangu.

Ninamshukuru sana Godlisten G.Kombe (Phd) Dean of Student College of Earth Science kwa sadaka yake iliyoniwezesha kuchapisha nakala za vitabu hivi.

Ninalishukuru kanisa la USCF-CCT-UDOM (KIPEKEE KITIVO CHA TIBA NA ELIMU) kwa jinsi lilivyothamini huduma hii na kuhakikisha linakua na kuenea maeneo mbalimbali na niliuona mchango wao wa hali na mali. Walikuwa mstari wa mbele kunisaidia nilipohisi kupungukuwa.

Mwisho kabisa ninamshukuru **Mwl Wilibath Thomas, Mwl Clinton Sanga, Brother Elibariki, mtumishi wa Mungu Elisha Ndile, Amani Simwinga, Faraja Mkilanya, Baaka Maliaki, Faibeth Mkilanya, Rehema Mauta, Mwl &Mwnj Baraka Shibanda**.

## UTANGULIZI

Mara nyingi tunadhani kwamba mtu anapofariki, wazazi wake au ndugu zake ndio wanaoandika historia yake, lakini ukweli ni kwamba wazazi au ndugu

wanaandika habari za huyo mtu ambazo yeye mwenyewe alishaiandika kwenye mioyo yao. Kwa maneno mengine ameshaweka alama au kumbukumbu kwenye mioyo ya hao watu. Na kila siku kwenye maisha tunakutana na vitu vipya, na kila kinachokuja kinagusa maisha yako kwa uzuri au ubaya. Ninasema hivi kwa sababu dunia tunayoishi tunakutana na vitu alivyoviumba Mungu ambavyo kwa asili yake ni vizuri na vikamilifu lakini kuna vile ambavyo tunaletewa na shetani na vinaonekana vibaya kama vile havikuumbwa na Mungu.

Suala la kuacha alama au kumbukumbu ni suala la muhimu sana kwa mtu binafsi, kwa jamii inayomzuka na kizazi kinachokuja. Ni suala lenye gharama na linalohitaji kujua sababu za kutaka kufanya hivyo, maana ni vigumu sana kuwa na moyo wa kufanya jambo usipojua sababu ya kufanya hivyo.

Mmoja ya mambo ya msingi ni kuhakikisha kuona kuwa leo yako ni bora kuliko jana. Ukiona jana ni bora kuliko leo, ujue leo hujafanya kitu. Mara nyingi tunapofanya uchaguzi wa viongozi katika maeneo mbalimbali, wanaoshinda ni wale wenye kibali kwa watu, na kilichowapa kibali ni walichofanya jana. Yaani historia waliyoandika kwenye mioyo ya watu waliowahi kuishi nao. Na wakati mwingine kuna viongozi walipigiwa kura bila kuomba au kufanya kampeni kwa sababu matendo yao yanawakilisha sifa zao. Na ndio maana utasikia uongozi wa Rais fulani au kiongozi fulani hatutausahau, kinachowafanya wasiusahau huo uongozi ni kile alichokifanya au kwa maana nyingine ni ile alama aliyoiacha akiwa kama kiongozi.

Watu wanaweza kukukumbuka kwa mabaya au mazuri, lakini hakuna sababu ya kukumbukwa kwa mabaya wakati Mungu alikuumba kwa mazuri na unauwezo wa kufanya hivo. Ingawa kuna wakati lina ugumu wake lakini ile kwamba lina ugumu haimainishi haliwezekani. Kuna msemo unaosema kuwa wema ni akiba, na ubaya pia ni akiba, **akiba ni kitu cha thamani kilichohifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya wakati ujao**. Kwa hiyo unapotenda wema unaweka huo wema uje utumike kwa wakati ujao

inawezekana usitumike tena kwako lakini utakuja kutumika hata kwa kizazi chako kinachokuja.

Alama ninayozungumzia ni alama nzuri au kumbukumbu nzuri itakayoishi miaka mingi na kuwasaidia wao kwenye maisha yao ya kila siku. Mungu anapokupa nafasi ya kuokoka ndani ya hiyo nafasi ameweka vitu vitatu.

**Jambo la kwanza.**

Mungu anakupa nafasi ya kuokoka kwa ajili yako mwenyewe. Kwa sababu unapata uzima wa milele katika Kristo Yesu na ndani ya wokovu kuna baraka ambazo zimeambatanishwa **Na hayo yote mtazidishiwa (Mathayo 6:33)**. Hizo baraka hatutumii mbinguni tunazitumia hapa duniani.

**Mathayo 19:27-29 Ndipo Petro akajibu akamwambia, tazama sisi tumeacha tukakufuata tutapata nini basi? Yesu akawaambia Amin nawaambia ya kwamba ninyi mlionifuata mimi, katika ulimwengu mpya atakapoketi mwana wa Adamu, katika kiti cha utukufu wake, ninyi nanyi mtaketi katika viti kumi na viwili mkiwahukumu mataifa kumi na mbili za Israel, Na kila mtu aliyeacha nyumba, au ndugu wa kiume au wa kike, au baba, au mama, au watoto, au mashamba, kwa ajili ya jina langu, atapokea mara mia, na kuurithi uzima wa milele.**

Si kwamba unapata wokovu peke yake ukiwa ndani ya Yesu, lakini pia maisha ya hapa duniani yanakaa sawa na kuwa ya mafanikio.

**Jambo la pili.**

Mungu anakupa nafasi ya kuokoka kwa ajili ya watu wake ambao hawajaokoka. Maandiko yanasema;

**Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa;**

**ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni (Yohana 15:16).**

Baada ya kuona sababu ya kwanza ya Mungu kutuokoa, Yesu Kristo mwenyewe anatuambia kuwa nimewachagua ninyi, nami nimewapa kazi ya kwenda kufanya, ambayo ni **kwenda kuzaa matunda, ambayo yatadumu (yatakaa).** Baada ya Mungu kutuokoa anataka tukaguse maisha ya watu wengine, tukiwahubiria habari njema inayowaleta kwa Kristo, na waendelee kuduma katika maisha ya kumjua Mungu.

**Basi, enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi, na tazama mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari (Mathayo 28:19).**

Bwana Yesu anawaambia wanafunzi wake (wakristo kwa sasa) kuwa mimi nimefufuka, na ninapaa kwenda mbinguni, lakini kazi ya kuwaokoa nimemaliza na kwa sababu hiyo nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani, ninawaachia kazi ninyi, kazi yenyewe ni hii, **enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,** akimaanisha enendeni mkabadilishe mfumo wa maisha ya watu, badala ya kuendelea kuishi maisha ya dhambi, wabadilike na kumtumikia Mungu.

Maandiko pia yanatuambia kuwa,

**Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo; mmepata bure, toeni bure (Mathayo 10:8).**

Yesu anazidi kutuonesha kuwa wokovu tulionao tumeupata bure, kwa hiyo tusisite kuutoa bure kwa wengine kwa maana ya kugusa maisha yao, anasema kwa wokovu niliowapa na kwa nguvu iliyopo ndani ya wokovu huo, enendeni kwa kondoo walioopotea wa nyumba ya Israel mfanye yafuatayo **Pozeni wagonjwa, fufueni wafu, takaseni wenye ukoma, toeni pepo.**

**Jambo la tatu.**

Mungu anakupa nafasi ya kuokoka kwa ajili ya yake mwenyewe. Biblia inasema hivi;

**Jueni kwamba Bwana ndiye Mungu; Ndiye aliyetuumba na sisi tu watu wake, Tu watu wake, na kondoo wa malisho yake (Zaburi 100:3).**

Kwa sababu tu mali yake, Mungu hayupo tayari kuona kazi ya mikono yake inapotea na kuharibika. Watu wote wanaoishi duniani wameumbwa na Mungu, hakuna aliyekuja mwenyewe, na kila aliyeumbwa na Mungu amekuja kwa kusudi maalum, hakuna aliyekuja duniani kwa bahati mbaya, na hilo kusudi anajua Mungu mwenyewe. Ukitaka kujua matumizi ya kitu muulize mtengenezaji wa hicho kitu. Hata kama unakiona kinafaa kwa matumizi unayodhani kuwa ni sahihi lakini uhalisia na ukweli wake anajua mtengenezaji wa hicho kitu.

Uhusiano wako na Mungu ni wa muhimu sana kwa sababu, bila kuwa na uhusiano mzuri na Mungu utatumika nje ya kusudi lake, utafanya ambavyo hajakuagiza kufanya, utatumia gharama na muda mahali ambapo hajakuagiza na utaenda kinyume na mpango wake kwako, na matokeo ya kwenda kinyume na mapenzi ya Mungu ni kuja kuacha alama yenye majuto kwa vizazi vinavyokuja baada yako. Lutu aliwahi kufanya kosa kama hilo pamoja na binti zake.

**Wakamnywesha baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka huyo mkubwa akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Ikawa siku ya pili, mkubwa akamwambia mdogo, Tazama, nimelala jana na baba yangu, tumnyweshe mvinyo tena usiku huu, ukaingie ukalale naye. Wakamnywesha tena baba yao mvinyo usiku ule, akaondoka mdogo akalala naye, wala yeye hana habari alipolala wala alipoondoka. Basi hao binti wote wawili wa Lutu wakapata mimba kwa baba yao. Yule mkubwa akazaa mwana, akamwita jina lake Moabu; huyo ndiye baba wa**

**Wamoabi, hata leo. Na yule mdogo naye akazaa mwana akamwita jina lake Benami; huyo ndiye baba wa Waamoni hata leo. (Mwanzo 19:33-38).**

Lutu alipewa maelekezo ya wapi pa kwenda, lakini akajichagulia mahali pa kwenda mwenyewe, malaika wakamruhusu (kumbuka ile kwamba wamemruhusu haimainishi alikuwa sahihi) ile nchi waliyokimbilia haikuwa na wanaume shida iliyopelekea binti zake kufanya hila kwa kumpa mvinyo wakalala naye. Shida ni matokeo yaliyokuja, binti mkubwa alipata ujauzito akamzaa Moabu na wa pili akamzaa Benani baba yao Waamoni.

Ukiwaacha wafilisti, miongoni mwa mataifa yaliyowatesa wana wa Israel ni **Wamoabu** na **Waamoni** ambao ni matokeo ya alama iliyoachwa na Lutu kwa kutokutii alichoambiwa na malaika. Na iliwachukua muda mrefu wana wa Israel kuwaondoa **Wamoabu** na **Waamoni.**

Ninatamani ujiulize ndani yako, Lutu aliyefanya hilo jambo hayupo, na historia yake iliishia palepale, mabinti zake waliokuwa chanzo nao hawapo na hatuna historia, lakini matokeo ya walichokifanya yanaendelea kuwepo na sio matokeo mazuri.

**Wana wa Israeli walimtumikia Egloni mfalme wa Moabu muda wa miaka kumi na minane (Waamuzi 3:14).**

Nina uhakika kabisa kama Lutu angejua haya yatakuja kutokea asingekataa maelekezo aliyopewa na malaika, lakini pia mabinti zake Lutu wasingeweza kufanya kitu kama kile. Ni muhimu sana kwako wewe kuhakikisha unaacha alama isiyo na majuto kwa kizazi kinachokuja.

Mambo yote aliyofanya Mungu na anayoendelea kufanya kuhusu mwanadamu yalifanyika kwa mikakati na maamuzi ya msingi sana, ndio maana wewe mi wa muhimu mbele zake na hii ndio sababu ya Mungu kudai mahusiano mazuri na wewe.

Na lengo la uhusiano mzuri ni kuhakikisha kusudi lake linatimia, na kazi yake itendeke kama alivyokusudia Mungu mwenyewe.

Mungu alituumba tufanyike kielelezo kwa wengine katika kumjua Yeye. Na maisha aliyotupa Mungu ni lazima yaguse maisha ya wengune waliopo chini yetu kwa namna ya kuwasaidia na kuwainua juu.

# SURA YA KWANZA

## *KWA NINI MUNGU ANATAKA MAHUSIANO MAZURI NA MWANADAMU?*

Zipo sababu nyingi zinazodai mahusiano yetu na Mungu. Kwa neema ya Mungu nimekuwekea baadhi ya hizo sababu na kuezielezea kwa kifupi.

### 1. UUMBAJI ULIFANYIKA BAADA YA KIKAO.

Mungu aliumba vitu vyote kwa neno lake, alikuwa akisema **na iwe** linakuwa kweli, kiasi kwamba hata mbingu na nchi viliumbwa kwa neno. Lakini lililpokuja suala la kumuumba mwanadamu Mungu aliitisha kikao kilichohusu namna na mfumo wa kumuumba mwanadamu, hii inatuonesha kuwa mwanadamu ni wa muhimu sana kuliko kiumbe alichowahi kukiumba.

**Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi.** (**Mwanzo 1:26)**

Mungu aliweka mfumo wa kiutawala na kiuongozi wa kimbingu uwepo hapa duniani, na utawale kwa jinsi ambavyo unatawala mbinguni, lakini utawala huu aliwapa wanadamu, ndio maana ya kusema **wakatawale.** Angeweza kuumba kila kitu na kutawala mwenyewe lakini alimheshimu mwanadamu na kumpa nafasi ya kutawala kila kitu alichokiumba. Kwa maneno mengine tungeweza kusema Mungu ametupa nafasi ya kukaimu utawala wake hapa duniani, kitu hicho kinatulazimu tuwe na ushirikiano mzuri na Mungu. Kwa kuwa taratibu za kutawala zimetoka kwake ni lazimu kupokea maelekezo kutoka kwake kuhusu jinsi gani ya kutawala.

Suala la kuwa na ushirikiano na mahusiano alilianzisha Mungu mwenyewe pale bustani ya Edeni, maana alikuwa akiwatembelea. Lengo la

kuwatembelea ni kuhakikisha kuwa kila siku kazi aliyowapa inaenda vizuri. Ndivyo ilivyo hata leo  kwetu Mungu ametupa kazi ya kuujenga ufalme wake hapa duniani na anapenda tuwe na mahusiano ya karibu naye ili kufanya kazi yake ifanikiwe hapa duniani.

**Mwanzo 3:8 Kisha wakasikia sauti ya Bwana Mungu, akitembea bustanini wakati wa jua kupunga; Adamu na mkewe wakajificha kati ya miti ya bustani, Bwana Mungu asiwaone.**

Biblia inatuambia kuwa Adamu na Eva walisikia sauti ya Bwana Mungu **akitembea bustanini**, hii inatuonesha kuwa Mungu alitenga muda maalum wa kuwatembea yaani kuhakikisha kuwa kuna ukaribu na Yeye kwa lengo la kutaka kujua wanaendeleaje na kazi aliyowapa pale bustanini.

## 2. WOKOVU ULIKUJA BAADA YA KIKAO.

Baada ya dahmbi kuingia duniani uhusiano wa mwanadamu na Mungu haukuwa mzuri kiasi cha Adamu kuondolewa katika busatni na kuwekewa ulinzi usio wa kawaida.

**Basi akamfukuza huyo mtu, akaweka Makerubi, upande wa mashariki wa bustani ya Edeni, na upanga wa moto uliogeuka huko na huko, kuilinda njia ya mti wa uzima (Mwanzo 3:24).**

Neno **alimfukuza** maana yake **alitumia nguvu** au **alimlazimisha** kuondoka pale bustanini, swali la kujiuliza ni kwamba, *kwa nini Mungu amfukuze mwanadamu aliyemuumba kwa mfano wake na kwa sura yake?* Maana yake kuna jambo halikwenda vizuri na kumfanya Mungu kuchukua maamuzi ya namna ile. Mungu alipoona kuwa uhusiano wake na mwanadamu umeondoka ilimlazimu afanye mkakati wa kuhakikisha mwanadamu anakauwa karibu nae.

Na huo mkakati wa wokovu wa mwanadamu ni mkakati uliofanywa mbinguni na Mungu mwenyewe kupitia Yesu Kristo.

**Isaya 6: 8 Kisha nikaisikia sauti ya Bwana, akisema, Nimtume nani, naye ni nani atakayekwenda kwa ajili yetu? Ndipo niliposema, Mimi hapa, nitume mimi.**

Mwanadamu pekee alijadiliwa hakuna kiumbe kingine chochote ambacho katika maisha yake iliwahi kuwekewa kikao Mbinguni. Wakati wa uumbaji tunaona kitu kama hiki, kwamba Na tumfanye mtu kwa mfano wetu na kwa sura yetu, na katika mikakati ya ukombozi wa wanadamu tunaona mazingira kama yale yale yakijirudia, kwamba nimtume nani, nae ni nani aende kwa ajili (kwa niaba yetu).

**Mathayo 1:21 Naye atazaa mwana, nawe utamwita jina lake Yesu, maana, yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao.**

Mpango wa kuja Yesu ulishaandaliwa na hata ujio wake ulijulikana lakini pia lengo la kuja lilikuwa bayana, **kuwaokoa watu wa Mungu na dhambi zao.**

Ikiwa Mungu alimtoa Yesu atuokoe na dhambi zetu, na akafanya hivyo basi kuna sababu za msingi za Mungu kudai mahusiano mazuri kwa mwanadamu aliyemuumba.

## 3. WASIOMJUA MUNGU WATAGEUZA MAWAZO MIOYO YAO.

Mara nyingi unapokuta hakuna maelewano katika eneo kuhusu suala la ibada, Mungu anatafuta namna ya kuifunua au kujidhihirisha ili watu wote wajue ya kuwa Yeye ndiye Mungu, ingawa ukweli ni kwamba Mungu ni Mungu, na anabaki kuwa Mungu hata kama kuna watu hawataki awe Mungu. Maana yake hata kabla hajajidhihirisha kwa hao wasiomjua alikuwa Mungu ila tatizo ni kwamba hawajaujua Uungu wake.

Rais wa nchi aliyechaguliwa kikatiba ni Rais kwa waliomchagua na kwa ambao hawajamchagua ni Rais kwa wanaomjua na wasiomjua, suala lakuja kujulikana kwa wasiomjua linahitaji utambulisho, na lazima awepo mtu wa kumtambulisha.

Tuangalie habari ya mtumishi wa Mungu Eliya:

**1Wafalme 18:36-39 Ikawa, wakati wa kutoa dhabihu ya jioni, Eliya nabii akakaribia, akasema, Ee Bwana, Mungu wa Ibrahimu, na wa Isaka, na wa Israeli, na ijulikane leo ya kuwa wewe ndiwe Mungu katika Israeli, na ya kuwa mimi ni mtumishi wako, na ya kuwa nimefanya mambo haya yote kwa neno lako. Unisikie, Ee Bwana, unisikie, ili watu hawa wajue ya kuwa wewe, Bwana, ndiwe Mungu, na ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie. Ndipo moto wa Bwana ukashuka, ukaiteketeza sadaka ya kuteketezwa, na kuni, na mawe, na mavumbi, ukayaramba yale maji yaliyokuwamo katika mfereji. Na watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi; wakasema, Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu.**

Mtumishi wa Mungu Eliya alifanya maombi yaliyoleta mabadiliko makubwa katika ulimwengu wa Roho na kubadilisha mfumo wa ibada wa eneo lile, kwa sababu alikuwa na uhusiano mzuri na Mungu.

**Unisikie, Ee Bwana, unisikie, ili watu hawa wajue ya kuwa wewe, Bwana, ndiwe Mungu, na ya kuwa wewe umewageuza moyo wakurudie. (1Wafalme 18:37)**

Mmoja ya malengo ya Mungu aliyoweka ndani ya moyo wa Eliya ni kuhakikisha manabii wa baali wanabadilisha mioyo yao na kumwelekea Mungu wa kweli. Na maombi haya yalijibiwa.

**Na watu wote walipoona, wakaanguka kifudifudi; wakasema, Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu.(1Wafalme 18:39).**

Natamani uone jinsi gani hawa manabii wa baali walikuwa hawana mpango kabisa na Mungu wa Eliya mpaka yalipofanyika maombi ya namna ile ya kumtambulisha Mungu katika eneo lile. Pamoja na kwamba Mungu alikuwepo katika eneo lile lakini hawa manabii wa baali walikuwa wanafanya ibada kwa miungu yao, hawakutambua uwepo wa Mungu. Ndipo mwishoni wanakuja kukubali kufanya ibada kwa Mungu wa kweli.

**Bwana ndiye Mungu, Bwana ndiye Mungu.**Huu ni msisitizo wa kuonesha jinsi gani Bwana ndiye Mungu.

Mara nyingi Mungu huwatumia watu ambao wana uhusiano mzuri na Yeye kujidhirisha kwa wale wasiomjua, kwa lengo la kuwabadilisha mioyo na kumwabudu Yeye peke yake.

**Daniel 3:4-5 Ndipo mpiga mbiu akapiga kelele akisema, Enyi watu wa kabila zote, na taifa, na lugha, mmeamriwa hivi, wakati mtakapoisikia sauti ya panda, na filimbi, na kinubi, na zeze, na santuri, na zomari, na namna zote za ngoma, lazima kuanguka na kuiabudu sanamu ya dhahabu, mfalme Nebukadreza aliyoisimamisha.**

Mfalme Nebukadreza alitengeneza sanamu na kuisimamisha,baada ya kuisimamisha aliwaita maamiri, manaibu, maliwali, makadhi, watunza hazina, mawaziri na wakuu wa wilaya zote. Kwa maana hiyo alihakikisha viongozi wote wa serikali wamehudhuria ibada hiyo muhimu, ili kuondoa upinzani wowote utakaojitokeza kuzuia au kupinga hiyo ibada. Na aliweka tangazo rasmi kuhusu hili jambo. Wakati Nebukadreza anafanya haya yote Mungu alikuwepo lakini alinyamaza akiwa anasubiri saa ya kujidhihirisha na kuwageuza mioyo yao. Na alihitaji mfalme mwenyewe ndiye aongoze mabadiliko ya sheria ya ibada. Mungu alitaka ajioneshe kwa watu wote kupitia vijana waaminifu walikubali kuweka vipaumbele vyao vya maisha yao kwa Mungu (waliokuwa kuwa tayari kuweka uhusiano mzuri na Mungu).

Nebukadreza hakuwa na mchezo kabisa katika suala la kuiabudu sanamu yake, maana alitangaza na adhabu itakayompata mtu yule asiyekuwa tayari kuiabudu sanamu.

**Daniel 3:6 Na kila mtu asiyeaniuka na kuabudu atatupwa saa iyo hiyo katika tanuru ya moto uwakao.**

Pamoja na uzito wa amri ya mfalme, akina Shadrack, Meshack na Abednego walibaki na msimamo wao kuwa hawapo tayari kufanya ibada hiyo iwe kuna adhabu au hakuna adhabu.Biblia inasema mfalme alikasirika sana.

**Ndipo Nebukadreza akajaa ghadhabu, na sura ya uso wake ikabadilika juu ya Shadraka, na Meshaki, na Abednego, basi akatoa amri watie moto ile tanuru mara saba kuliko desturi yake ya kutiwa moto. (Daniel 3:19).**

Ingawaje adhabu iliongezwa mara saba, hawa watumishi walibaki na msimami wao katika Kristo, maana alikuja kuwaokoa motoni. Lengo la Nebukadreza ilikuwa ni kuhakikisha kuwa eneo lile linakuwa na aina moja ya ibada ambayo ni kuabudu  sanamu wake,lakini mwishoni Mungu alipoamua kujidhihirisha mbele ya watu wote kwa kuwalinda wasiteketee kwenye moto ilimlazimu mfalme abadili maamuzi na sheria na watu wote wakamwabudu Mungu wa akina Shadrak, Meshaki na Abednego.

Kitu gani ninakusudia ukifahamu? Shetani anaweza kukubana usiweze kusimama kwenye nafasi yako uliyopewa na Mungu ili kumtambulisha kwenye hilo eneo ili watu wasimwabudu Mungu wa kweli.

Angalia habari nyingine iliyowahi kubadilisha mfumo wa ibada wa watu wote kupitia maombi ya mtumishi Daniel aliyekuwa na uhusiano mzuri na Mungu.

**Ndipo mfalme Dario akawaandikia watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, waliokaa juu ya uso wa dunia; Amani na iongezeke kwenu, Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli; maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme wake ni ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho.**

Kabla mfalme Dario hajatoa agizo au amri  kwamba Mungu wa Daniel ndiye Mungu anayepaswa kuabudiwa peke yake, Mungu alikuwa ni Mungu, shida ilikuwa hawajamtambua kama ndiye Mungu, na Mungu alisubiri saa ambayo watu wote kupitia mfalme watasikia amri na kuanza kumwabudu kama Mungu.

Uhusaino wa mtu na Mungu unaweza kumfanya Mungu atambulike mahali anapokaa huyo mtu na kuabudiwa kama ndiye Mungu.

## 4. UNAPATA NAFASI YA KUKAA CHINI YA UONGOZI WA ROHO MTAKATIFU.

**Zaburi 143:10 Unifundishe kuyatenda mapenzi yako, Kwa maana ndiwe Mungu wangu; Roho yako mwema aniongoze kwenye nchi sawa.**

Roho Mtakatifu ni dira ya maisha ya Mkristo, ndiye anayetoa mwongozo wapi pa kwenda na wapi pa kutokwenda, nini cha kufanya na nini sio cha kufanya, nini cha kusema na nini sio cha kusema na wakati wa kufanya hayo yote.

Ukubwa wa meli au ndege hauwezi kuwa sababu ya meli au ndege kutokupotea, ikiwa dira itakosekana. Mwongozo unaotolewa na dira humsaidia nahodha au rubani kufika mwisho wa safari bila kupotea.

Roho Mtakatifu ni mwangalizi wa kila kazi ya Mungu tunayoifanya hapa duniani. Biblia inatufundisha kuwa,

**Lakini kila mmoja hupewa ufunuo wa Roho kwa kufaidiana. Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima; na mwingine neno la maarifa, apendavyo Roho yeye yule; mwingine imani katika Roho yeye yule; na mwingine karama za kuponya katika Roho yule mmoja; na mwingine matendo ya miujiza; na mwingine unabii; na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za lugha; na mwingine tafsiri za lugha; lakini kazi hizi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye.** 1**Wakorintho 12:8 -11**

Kuongozwa na Roho Mtakatifu ni jambo la muhimu sana katika maisha ya wokovu, na katika hali ya kuongozwa maelewano ni ya msingi sana, inapotokea hakuna maelewano ni vigumu kupokea maelekezo ya anayekuongoza. Mungu anataka mahusiano yetu na Yeye yawe vizuri na yaendelee kudumu ili apate nafasi ya kutuongoza kupitia Roho Mtakatifu.

Biblia inatuambia kuwa;

**Kwa kuwa wote wanaoongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu (Warumi 8:14).**

Roho wa Mungu maana yake Roho Mtakatifu, ndiye aliyepewa dhamana ya kuwaongoza wana wa Mungu. Kuna tofauti kati ya wana wa Mungu (watoto wa Mungu) na watu wa Mungu. Kila mtu ni wa Mungu, lakini nafasi ya kuitwa wana wa Mungu wamepewa waaminio kulingana na injili ya Yohana **Alikuja kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake (Yohana 1:11-12).**

Imani inayotufanya kuwa wana ni imani tuliyo nayo katika Kristo Yesu. Kama biblia inavyosema:

**Kwa kuwa ninyi nyote mmekuwa wana wa Mungu kwa njia ya imani katika Kristo Yesu (Galatia 3:26).**

Biblia inatufundisha wazi kwamba kilichotufanya kuwa wana ni imani katika Kristo, kwa hiyo wanaohusika hapa ni walio katika Kristo. Pamoja na kwamba Mungu aliwaumba watu wote tena kwa mfano wake na kwa sura yake lakini kuna jambola ziada Yesu alifanya kwetu. Alikuja kutufanya tuwe watoto wa Mungu kwa njia ya imani.

**Tazameni, ni pendo la namna gani alilotupa Baba, kwamba tuitwe wana wa Mungu; na ndivyo tulivyo. Kwa sababu hii ulimwengu hautuTambui, kwa kuwa haukumtambua yeye (1Yohana 3:1).**

Kulingana na huo mstari hapo juu, kama umefanywa mwana, ulimwengu hauwezi kukutambua kwa sababu haukumtambua aliyekufanya kuwa mwana.

Baada ya kuwa tumeokoka na kufanywa kuwa wana wa Mungu, Mungu anahitaji kutuongoza kupitia Roho wake Mtakatifu

Zipo sababu nyingi kwa nini Mungu anataka kutuongoza kupitia Roho Mtakatifu. Zifuatazo ni baadhi ya sababu hizo;

### *(a) Yesu Kristo mwenyewe Aliongozwa na Roho Mtakatifu.*

Tujiulize swali hili la msingi sana, kwa nini Bwana Yesu ambaye ni Mungu kamili ndani yake alikuwa akiomba kwa bidii sana kuwazidi hata wanafunzi wake? Na si kuomba tu, alikuwa akifunga. Na biblia inatufundisha pia kuwa Yesu alikuwa akiongozwa na Roho.

**Luka 4:1 Na Yesu, hali amejaa Roho Mtakatifu, alirudi kutoka Yordani, akaongozwa na Roho muda wa siku arobaini nyikani.**

Kama Yesu alikuwa anaongozwa na Roho Mtakatifu basi hakuna namna sisi tutakwepa kukaa chini ya uongozi wa Roho Mtakatifu. Hii ni kufuata alichokuwa akifanya Bwana wetu kama kielelzo kwetu na kushika maagizo yake.

### *(b) Ili tusizitii tamaa za mwili.*

**Warumi 8:7-8 Kwa kuwa ile nia ya mwili ni uadui juu ya Mungu, kwa maana haitii sheria ya Mungu, wala haiwezi kuitii. Wale waufuatao mwili hawawezi kumpendeza Mungu.**

Basi nasema enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili.Tunatakiwa tuenende kwa Roho ili tusizitimize tamaa za mwili. Siku zote mwili na Roho ni maadui nia ya mwili ni mauti na nia ya Roho ni uzima na amani (**Warumi 8:7).** Maana yake siku zote mwili utakuongoza kufanya mambo ambayo mwisho wake ni mauti ya mwili na kiroho pia. Mwili wako unakuandaa wewe kukaa mbele ya kiti cha hukumu na kuhukumiwa adhabu. Na ndio maana mwili haujawahi kuwa rafiki wa jambo lolote la kiroho, ukitaka kufunga mwili utakuwa kinyume na wewe, ukitaka kuomba mwili utakuwa kinyume na wewe, ukitaka kwenda ibadani mwili utakupa sababu nyingi mno

za kutokwenda ibadani kwa sababu hauna mpango kabisa wa kwenda mbinguni.

Sasa utakapoongozwa na Roho Mtakatifu utaratibu wake utakuacha huru mbali na hayo mambo ya mwili na utakuongoza katika uzima na amani na kulitenda tunda la Roho ambalo ni;**Upendo, Furaha, Amani, Uvumilivu Utu Wema, Fadhii, Uaminifu, Upole Na Kiasi (Wagalatia 5:22-23)**

***(c) Ili tupate kuyaelewa mafumbo ya Mungu na kuyafasiri mambo ya Rohoni kwa jinsi ya Rohoni.***

**Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho, maana Roho huchunguza yote hasa mafumbo ya Mungu (1Wakorinto 2:10).**

Roho ndiye anayejua makusudi ya Mungu kwetu na**mafumbo ya Mungu** au **siri za Mungu** ambayo sisi peke yetu hatuwezi kufahamu, ila yeye anapokaa ndani yetu **anatufunuliwaau anaweka wazi.**

Bibili inasema kwamba;

**Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya Rohoni kwa maneno ya Rohoni** (**1Wakorinto 2:13)**

Hapa najua walio wachungaji, walimu wa neno la Mungu au viongozi wa vikundi mbalimbali vya kiroho watanielewa zaidi. Naomba unielewe vizuri mtu wa Mungu, Roho Mtakatifu ndiye mwenye uwezo wa kuchunguza kilichopo kwenye ufahamu wa Mungu kuhusu wewe, ndoa yako, kanisa lako, biashara yako, masomo yako, nchi yako huduma yako, ujana wako, changamoto zako unazopitia na kila jambo usilolielewa wewe Mungu anajua na anatamani na

wewe ujue pia. Na hii kazi anaifanya Roho Mtakatifu anachukua hizo siri na kutujulisha sisi. Pia Roho Mtakatifu ndiye anayekusaidia kuyanena, kuyafundisha au kuyafafanua maneno ya Mungu kwa watu wake, anaposema kuyafasiri maana yake kuyafundisha mambo ya Rohoni kwa jinsi au namna ya Rohoni.

Hivyo kama wewe ni kiongozi au mwalimu wa neno la Mungu, ukiongozwa na Roho, yeye atakuongoza au atakusaidia kuwafundisha hao watu neno la Mungu kwa jinsi ya Rohoni yaani kwa mfumo wa Rohoni kulingana na watu ulio nao, maana yeye ndio mtunzi wa hilo Neno.

Biblia pia inazidi kutufundisha kuwa:

**Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu, bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu (2Petro 2:21).**

Wakiongozwa na Roho, maana yake, walipokea maelekezo au mwongozo wa kutoa unabii (neno la Mungu) kutoka kwa Mungu kupitia Roho Mtakatifu. Na ndio maana kama wewe ni mtumishi wa Mungu unayewadumia watu wake kwa njia ya neno, ni muhimu sana ukajua nafasi ya Roho Mtakatifu katika huduma yako. Kumbuka unawahudumia watu wa Mungu, na unachowapa ni cha chake yaani cha Mungu, na ili uweze kupata hicho ili kuwapelekea watu wake ni lazima uwe na Roho Mtakatifu, ikitokea hayupo uwe na uhakika unachowapa sio cha Mungu, ni cha kwako.

### *(d) Ili tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu.*

**Lakini sisi hatukuipokea roho ya dunia, bali Roho atokaye kwa Mungu, makusudi tupate kuyajua tuliyokirimiwa na Mungu. Nayo twayanena, si kwa maneno yanayofundishwa kwa hekima ya kibinadamu, bali yanayofundishwa na Roho, tukiyafasiri mambo ya rohoni kwa maneno ya rohoni. Basi mwanadamu wa tabia ya asili hayapokei mambo ya Roho wa Mungu; maana kwake huyo ni upuzi, wala hawezi kuyafahamu, kwa kuwa yatambulikana kwa jinsi ya rohoni (IWakorintho 2:12-14).**

Sio kila mtu anaweza kufahamu ni kitu gani amepewa na Mungu ndani yake isipokuwa yule ambaye Roho Mtakatifu yuko ndani yake. Unapoongozwa na Roho Mtakatifu ndipo anapokusaidia kujijua wewe mwenyewe vizuri. Ndio maana anasema upate kuyajua yale ambayo Mungu amekupa katika maisha yako.

Roho Mtakatifu atakusaidia kujua aina ya vipawa ulivyonavyo, karama za Rohoni ulizonazo, huduma ulizonazo kama umeitwa huko, atakusaidia kujua vizuri unaweza kufanya nini na nini huwezi, kipi ufanye na kipi usifanye, atakusaidia kujua baraka zako za kiroho na kimwili pia. Kwa kifupi atakusidia kulijua kusudi la Mungu katika maisha yako na ufanye nini ili uweze kulifikia hilo kusudi na zaidi atakupa upako au nguvu za kuweza kuyapokea yale yote anayo kuagiza ili uweze kulifikia kusudi lake kwako na kuzirithi barakazako.

*(e)* ***Ili atusidie kuomba itupasavyo (sawasawa na mapenzi ya Mungu)***

Bibilia inasema:

**Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba jinsi itupasavyo, lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa (Warumi 8:26).**

Neno **itupasavyo** maana yake ni **sawasawa na au inavyotakiwa kuwa,** kwa hiyo kama Roho ndiye anayetufanya tuomba ipasavyo, maana yake peke yetu tukiomba tunaomba isivyopasa. Ila tukiomba na Roho Mtakatifu akiwa ndani yetu anatusaidia kuomba sawasawa, yaani ipasavyo.

Mmoja ya sababu ya maombi kutokujibiwa ni kutokuomba sawasawa na mapenzi ya Mungu, kinachosababisha tusiombe sawa sawa ni madhaifu au mapungufu tuliyo nayo katika maombi. Kazi ya Roho Mtakatifu ni kuhakikisha

sisi tumeomba sawa sawa na kile ambacho Mungu anataka tuombe (mapenzi ya Mungu). Sababu za Roho kuwa msaidizi wetu kwenye eneo la maombi kwa sababu Yeye anajua mapenzi ya Mungu. Mungu alipoliona hili ya kuwa hatuwezi kufahamu siri zake peke yetu, aliamua kutuwekea msaidizi ili awe anatujulisha siri zake na kila tuombapo tuombe sawasawa na mapenzi yake.

Serikali au shirika likitangaza nafasi za kazi linatoa maelekezo au utaratibu wa jinsi ya kufanya maombi sahihi kwa ajili ya hizo nafasi, watakaochaguliwa ni wale walioomba kwa kufuata maelekezo yaliyotolewa kulingana na hizo nafasi. Na inawezekana una sifa kabisa za kupata hiyo nafasi ya kazi, lakini kwa sababu ya kutokuomba kwa kufuata maelekezo unaweza kukosa. Wakati mwingine inawezekana hujui ni maelekezo gani yametolewa ili upate hiyo nafasi na ili upate hayo maelekezo unawatafuta wakala au ofisi zao ili upate maelekezo ya ya jinsi gani ya kuomba sawasawa. Watu wote wana sifa za kwenda mbele za Mungu na kuomba lakini sio wote wanaojibiwa, shida sio aina ya maombi, ni maelekezo kuhusu maombi wanayofanya. Na ili kupata maelekezo ni lazima awepo Roho Mtakatifu atakayekupa hayo maelekezo maana ndio anayefahamu.

Uongozi wa Roho Mtakatifu si kwamba unatusaidia tu kuomba sawasawa lakini pia uongozi huo unatufundisha namna au jinsi ya kuomba hayo mapenzi ya Mungu.Roho Mtakatifu anatufundisha kuhusu kuomba yaliyo mapenzi ya Mungu, lakini pia anatufundisha kuhusu namna ya kuomba hayo mapenzi ya Mungu, unaweza kufahamu kuwa hili jambo ni mapenzi ya Mungu, lakini ikakupa shida wakati wa kukiombea hapo ndipo Roho Mtakatifu anapoingilia kati.

### *(f) Ili atuongoze katika kufanya maamuzi.*

Kufanya maamuzi ni sehemu ya maisha ya mwanadamu.
Yapo maamuzi mengi sana ambayo mwanadamu anatakiwa kufanya kila siku na hakuna namna atakwepa kuyafanya.

**Warumi 8:1-2 "Sasa, basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika kristo Yesu imeniacha huru,mbali na sheria ya dhambi na mauti"**

Kwa sababu hiyo Mungu ametupatia Roho Mtakatifu ili atusaidie katika kufanya maamuzi. Roho Mtakatifu anapokuwa kiongozi anakupa uhuru juu ya kufanya maamuzi katika maisha yako. Sasa yeye anakuletea uhuru ndani wa kufanya jambo ambalo anajua ni la mafaniko kwako. Kumbuka siku zote nia ya Roho ni uzima na amani. Kwa hiyo kama Roho Mtakatifu atakosekana ndani yako uwe na uhakika utakosa uhuru wa kufanya maamuzi yatakayokupa amani. Hapa tunazungumzia maamuzi ambayo ukifanya utafurahia wewe, watu wanaokuzunguka na Mungu pia atafurahia.

**Basi Bwana ndiye Roho, walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru" (2Wakorinto 3:17**).

Zaidi ya kukupa uhuru wa kufanya maamuzi katika maisha yako binafsi, Roho wa Bwana akiwepo eneo fulani panakuwa na uhuru, na kama kuna uhuru basi hata yatayofanyika hapo yatakuwa huru.

Huenda ziko sababu nyingi zinazoelezea kwa nini unatakiwa uenende kwa Roho, lakini hizi chache ndizo Mungu alizonipa tuweze kushirikiana kujifunza. Ni imani yangu kwamba utakapoamua kutaka na kupenda kuongozwa na Roho ndipo utakapoona Mungu akijifunua kwako.
Kila mahali kunapokuwa na mahusiano mazuri, kunakuwa na mawasiliano mazuri pia mawasiliano kati yetu na Mungu ni kwa njia ya maombi. Ili

mahusiano yaendelee vizuri ni lazima mawasiliano yalete matokeo mazuri, yaani maombi yalete majibu mazuri.

## MAMBO YA MSINGI YATAKAYOKUSAIDIA KUACHA ALAMA.

### 1. UTII NA UNYENYEKEVU.

**Unyenyekevu ni**hali ya kuonesha utii au heshima kwa mtu au jambo.Unyenyekevu ni tabia na mfumo wa maisha ambao mtu anajiona yeye sio bora kuliko mwingine (si katika matokeo ya kazi yake bali katika kuthamini uwepo wao).

Unyenyekevu huanza ndani ya moyo wa mtu na sio katika vitendo vya nje, kiini cha unyenyekevu ni katika nia, fikra na mtazamo.

Mungu anapendezwa sana na watu ambao ni wanyenyekevu au wenye moyo wa unyenyekevu;

**Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake. Kila mtu asiangalie mambo yake mwenyewe, bali kila mtu aangalie mambo ya wengine. Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu (Wafilipi 2:2-9).**

Bibli pia inazidi kutufundisha ni kwa jinsi gani Mungu anapenda moyo wa unyenyekevu.

**Kwa sababu Mungu huwapinga wenye kiburi ,lakini huwapa wanyenyekevu Neema Basi nyenyekeeni chini ya mkono wa Mungu ulio, hodari, ili awakweze kwa wakati wake (1Petro 5:5b-6).**

Unapokuwa mnyenyekevu na kuwa mtii mbele za Mungu unaweza ukafanya jambo la tofauti na la kipekee litakaloweza kuwa kumbukumbu kwa kizazi chako. Unaposhindwa kuwa mtii na mnyenyekevu unahatarisha kizazi chako. Biblia inatufundisha watu ambao walihatarisha kizazi chao kwa kutokutii.

**Naye Yoshua akawaapisha kiapo wakati ule, akisema, Na alaaniwe mtu yule atayeinuka na kujenge tena mji huu wa Yeriko; ataweka msingi wake kwa kufiliwa na mzaliwa wa kwanza wake, tena atayasimamisha malango yake kwa kufiliwa na mtoto wake mwanamume aliye mdogo (Yoshua 6:26).**

Baada ya kutokutii sauti ya Mungu kupitia mtumishi wa Mungu Yoshua, Hieli Mbetheli alifiwa na watoto wake Biblia inasema;

**Katika siku zake Hieli Mbetheliakajenga Yeriko; akatia misingi yake kwa kufiwa na Abiramu mzaliwa wake wa kwanza, na kuyaweka malango yake kwa kufiwa na mwana wake mdogo Segubu; sawasawa na neno la Bwana alilolinena kwa Yoshua mwana wa Nuni (1Wafalme 16:34).**

## 2. TAMBUA NA KUBALI KUWA WEWE NDIYO UNATAKIWA KUACHA ALAMA.

Watu wengi wanaelewa kwa nini wako duniani lakini kwa sababu tuko wengi wanadhani suala la kuacha alama linawahusu watu fulani maalum kitu ambacho sio sahihi. Esta angesubiri jeshi la wayahudi lifanye mpango wa kujikomboa wokovu usingepatikana. Lakini alitambua na kukubali kuwa ile kazi inamhusu na alianza kulifanyia kazi kwa njia ya maombi. Unapaswa kwanza kutambua na kukubali kwamba hakuna mwingine anayepaswa kufanya hivyo zaidi yako.

**Nae Mordekai akawagiza wampelekee Esta jibu la kusema kuwa; Wewe usijidhanie kuwa wewe utaokoka nyumbani mwa mfalme zaidi ya wayahudi wote maana ukinyamaza kabisa wewe wakati huu ndipo**

**kutakapowatokea wahayudi msaada kwa njia nyingine ila wewe utaangamia pamoja na mlango wa baba yako.**

Natamani uone ni jinsi gani ambavyo Esta asingetambua na kukubali kuwa yeye ndio anatakiwa aache alama kwa njia ya kuwakomboa wayahudi wote wangekuwa kwenye wakati mgumu.

### 3. AMUA KWA DHATI KUTIMIZA KUSUDI LA MUNGU.

Mungu alipoweka kusudi lake ndani ya mwanadamu alijua kuwa atalitumikia vizuri, na hata kwetu sisi Mungu anategemea kuona kuwa tunalitumikia vizuri. Kulitumikia kusudi vizuri kutakufanya uweze kuacha alama nzuri isiyo na majuto. Na hii hutegemea maamuzi ya dhati aliyonayo mtu huyo juu ya hilo kusudi alilopewa na Mungu.

Biblia inatufundisha kwa habari za watoto wawili wa mzee Eli aliyekuwa kuhani, na watoto wake wakawa makuhani pia. Lakini hawakuamua kulitumikia kusudi la Mungu kwa uaminifu na walikuja kuleta majuto ndani ya taifa la Israel, yaani waliacha alama mbaya badala ya alama nzuri. Waliondoa nafasi ya kikuhani ndani ya familia ya mzee Eli. Mtoto aliyezaliwa na mkwewe Eli ambaye ilitakiwa awe kuhani katika Israel aliitwa **Ikabodi** yaani utukufu umeondoka ndani ya nyumba ya Israel na hao watoto wa Eli walikufa.

**Akamwita mtoto, Ikabodi, akisema Huo utukufu umeondoka katika Israel; kwa sababu sanduku la Bwana limechukuliwa na kwa sababu ya mkwewe na mumewe (1Samweli 4:21).**

Umewahi kujiuliza mtoto aliyetakiwa kuwa kuhani anaitwa jina majuto yaani alama mbaya, na hatakiwi tena kuwa kuhani kwa ajili ya hilo jina.

### 4. TUMIA KILA FURSA INAYOKUJA MBELE ZAKO KWA UMAKINI.

Kila fursa au nafasi unayopata imebeba jambo la KiMungu litakalokuwezesha kuacha alama au kuweka kumbukumbuku nzuri katika maisha ya watu wanaofuata baada yako.

Tunazidi kujifunza kutoka kwa Esta kuwa ilikuwa nafasi yake pekee kuahikisha kuwa wayahudi wanapata wokovu kupitia nafasi yake aliyopata kuwepo ndani ya jumba la kifalme na aliitumia vizuri.

**Basi Esta akawatuma wamjibu Mordekai, Uende ukawakusanye wayahudi wote waliopo hapa Shushani mkafunge kwa ajili yangu, msile wala kunywa muda wa siku tatu, usiku wala mchana, mimi na wajakazi wangu tutafunga pia, kisha nitaingia kwa mfalme (Esta 4:15-17).**

# SURA YA PILI

## *ILI MAOMBI YAJIBIWE*

**Maombi** ni mawasiliano kati ya mtu na Mungu. Ni kumweleza Mungu kile ulicho nacho moyoni mwako. Nasema kumweleza Mungu kwa maana hata yale tusiyomwambia anajua lakini inakuwa sio maombi. Kwa sababu maombi (mawasiliano) hayo yanahusu pande mbili, kumwambia Mungu na kumsikia Mungu anachosema. Maombi yote yalilenga kujibiwa, hakuna ombi ambalo Mungu ameruhusu halafu hana mpango wa kujibu.

Kanisa lisiloomba ni kanisa lisilo na nguvu, vivyo hivyo mtu (mkristo) yeyote asiyeomba ni mkristo asiye na nguvu naamanisha nguvu za kiroho. Kwa sababu kadiri unavyoomba ukiwa na imani kwa unachokiomba ndivyo unavyozidi kupokea, ikiwa utaacha kuomba ni hakika kiwango cha kupokea kitapungua. Kadiri tunavyoomba ndivyo tunavyopokea na kadiri tusivyoomba ndivyo hivyo tusivyopokea kutoka kwa Bwana.

**Mathayo 7:7-8 Ombeni, nanyi mtapewa……………Kwa maana kila aombaye hupokea.**

Huu mstari unatupa uhakika ya kwamba kwa sababu tu tunaomba tunaamini kuwa tutapokea, haya ni mafundisho ya awali kabisa ya Bwana Yesu wakati anaanza huduma, na mmoja ya eneo ambalo ameliwekea msisitizo ni kwenye kupokea (kupewa) kunakotokana na maombi.

Lakini jambo lingine la muhimu hapa ni kutambua kuwa biblia haijataja watu maalum wanaotakiwa kuomba.

Ndio maana Yesu akasema kila aombaye hupewa.Mara nyingi watu wanapofika kuomba mbele za Mungu wanakuwa makini na kuhakikisha kuwa kile wanachokihitaji kimefika kwa Mungu, bila kufikiri Mungu atasema nini kuhusu majibu ya maombi yao.

Maombi ni mwaliko kutoka kwa Mungu, kutualika mbele zake kwa ajili ya kuzungumza naye. Lakini pia mtu yeyote asiyeomba anatenda dhambi mbele za Mungu kama Biblia ianvyosema katika;

**Walakini mimi, hasha! Nisimtende Bwana dhambi kwa kuacha kuwaombea ninyi; lakini nitawaelimisha katika njia iliyo njema, na kunyoka (1Samweli 12:23).**

Kwa hiyo tunapoomba tunatimiza wajibu wetu kibiblia.

## MAMBO YANAYOFANYA MAOMBI YAKO YAJIBIWE.

## 1. UAMINIFU NA UNYENYEKEVU.

Mmoja ya vitu anavyochukia Mungu kwa wanadamu ni kijiinua na kiburi, lakini anapenda sana unyenyenkevu. Watu wote waliowahi kujiinua Mungu aliwachukulia adhabu kali lakini walipojidhili na kunyenyekea aliwapa kibali cha kusimama mbele zake tena.

Kuna wakati wana wa Israel walimkosea Mungu, akawatia kwenye mikono ya adui zao, wakamlilia ili awaponye lakini wakati huo hawajaondoa miungu ya kigeni kati yao. Walikuwa wanamwomba Mungu awaokoe lakini hawakuwa waaminifu na watiifu kwa maana walitakiwa kuondoa miungu ya kigeni kwanza ili kuonyesha utii wao na unyenyekevu wao mbele za Mungu. Walipoondoa miungu ya kigeni na kunyenyekea Mungu aliwasamehe.

**Nao wakaiondoa hiyo miungu ya kigeni iliyokuwa kati yao, nao wakamtumikia Bwana; na roho yake ilihuzunika kwa sababu ya msiba wa Israeli (Waamuzi 10:16).**

Kilichomsukuma Mungu kuachilia msamaha ni kile kitendo cha kuonyesha unyenyekevu wao na utii kwa Mungu na kukubali kuondoa miungu ya kigeni. Mungu huwapinga wenye kiburi bali wanyenyekevu huwapa neema, kwa sababu mtu yeyote anayejiinua anataka kuchukua nafasi yake ndio maana Mungu huwapinga.

Habari za mfalme Ahabu inatupa fundisho nzuri sana,

**Ikawa, Ahabu alipoyasikia maneno hayo, akayararua mavazi yake, akavaa magunia mwilini mwake, akafunga, akajilaza juu ya magunia, akaenda kwa upole. Neno la Bwana likaja kwa Eliya Mtishbi, kusema, Huoni jinsi Ahabu alivyojidhili mbele yangu? Basi kwa sababu amejidhili mbele yangu, sitayaleta yale mabaya katika siku zake; ila katika siku za mwanawe nitayaleta mabaya hayo juu ya nyumba yake (1Wafalme 21:27-29).**

Mfalme Ahabu ni mmoja ya wafalme waliofanya mabaya mbele za Bwana, kwa kuwa hakuwa tayari kumsikia Mungu na kuzifuata sheria zake katika uongozi wake, (**1Wafalme 21:25 Lakini hapakuwa na mtu kama Ahabu, aliyejiuza atende maovu machoni pa Bwana ambaye Yezebeli mkewe alimchochea).**

Pamoja na kuwa mfalme Ahabu ndiye mfalme aliyefanya mabaya mbele za Bwana na kumchukiza Mungu, alipoamua kujinyenyekeza Mungu akaamua kumsamehe.

Angalia kitu alichokuwa amekusudia Mungu juu yake:

**Angalia, nitaleta mabaya juu yako; nami nitakuangamiza kabisa, nitamkatia Ahabu kila mume, aliyefungwa na aliyeachwa katika Israeli. Kisha nitaifanya nyumba yako iwe kama nyumba ya Yeroboamu mwana wa Nebati, na kama nyumba ya Baasha mwana wa Ahiya, kwa ajili ya chukizo ulilonichukiza, hata kunighadhibisha, ukawakosesha Israeli. Tena Bwana alinena habari za Yezebeli, akisema, Mbwa watamla Yezebeli katika kiwanja cha Yezreeli. Mtu wa nyumba ya Ahabu afaye mjini, mbwa watamla, na yeye afaye mashambani ndege wa angani watamla(1Wafalme 21:21-24).**

Hii ni adhabu kali aliyokuwa amekusudia Mungu juu ya Ahabu, lakini alipoamua kujidhili na kunyenyekea kwa Mungu alisamehewa.

Kwa hiyo unapokuwa mtii na mnyenyekevu kwa Mungu, unapata kibali cha kusikilizwa na Mungu na kukupa neema ya kupokea majibu yako kutoka kwa Bwana.

## 2. IMANI.

Imani ni kiungo muhimu katika kuhakikisha maombi yako yanajibiwa, na ndio daraja analotumia Mungu kujibu maombi yetu. Imani haifanyi mambo kuwa mepesi bali inafanya mambo yanawezekana. Kwa sababu imani ni hakika ya

mambo yatarajiwayo kulingana na **Waebrania 11:1 Basi imani ni kuwa na hakika ya mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana.**

Maana yake imani ni udhihirisho au uthibitisho wa vitu ambavyo kwa macho ya kawaida hayaonekani. Uwezo ule wa kuona yasiyoonekana ndio unaoitwa imani.

Biblia inaweka wazi kuwa ikiwa hatuna imani kwa Mungu maombi yetu hayana kazi maana hayatajibiwa.

**Ila na aombe kwa imani, pasipo shaka yo yote; maana mwenye shaka ni kama wimbi la bahari lililochukuliwa na upepo, na kupeperushwa huku na huku. Maana mtu kama yule asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana. Mtu wa nia mbili husita-sita katika njia zake zote (Yakobo 1:6-8)**

Tunaona kwenye hiyo mistari kwamba ikiwa mtu ameamua kuomba basi **aombe kwa imani,** tena anapoomba kwa imani **asione shaka ndani yake,** lengo ni kutaka kuona unamtegemea Mungu kwa kila jambo na kumwamini kwa maana asiyeomba kwa imani na anayeona shaka ndani yake **asidhani ya kuwa atapokea kitu kwa Bwana.**

Huu ni mstari unaoweza kukupa kufanya maamuzi ya kuendelea kuomba au kutokuendelea kuomba kwa maana unaweka bayana, matokeo ya kuomba pasipo imani.

Nafasi ya imani ni kubwa sana katika kujibiwa maombi kwa sababu tunaangalia na kuweka mawazo yetu kuwa Mungu atafanya kile alichotuambia kuwa atafanya (**Kuhusu namna maombi yako yanavyoweza kujibiwa kupitia Imani unaweza kupata nakala ya kitabu changu cha IMANI ITENDAYO KAZI NDANI YETU).**

## 3. KUFUNGA.

Lengo la maombi ya kufunga ni kuunyamazisha mwili na kuuruhusu ulimwengu wa roho kufanya yaliyo mapenzi ya Mungu, Biblia inasema :

**Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili. Kwa sababu mwili hutamani ukishindana na Roho, na Roho kushindana na mwili; kwa maana hizi zimepingana, hata hamwezi kufanya mnayotaka (Wagalatia 5:16-17).**

Mwili hauwezi kuwa rafiki wa roho maana mahitaji yao hayalingani, kwa hiyo ili uweze kusimama na kuwa imara inategemeana na kipi kina nguvu kati ya mwili na roho. Ikiwa mwili utakuwa na nguvu na kuishinda roho yako ujue ni vigumu kutimiza mapenzi ya Mungu kwa njia ya maombi.

**Na hao walio wa Kristo Yesu wameusulibisha mwili pamoja na mawazo yake mabaya na tamaa zake (Wagalatia 5:24).**

Mtu anapofunga anatoa kipaumbele kwa mambo ya rohoni kufanikiwa zaidi kuliko mambo ya mwilini, na katika kutanguliza mambo ya kiroho ni muhimu sana kila mtu akajua kuuweza mwili wake na kuutisha katika utakatifu kulingana na (**1Wathesalonike 4:4).**

Biblia pia inatuonesha nafasi ya maombi ya kufunga.

**Wakakusanyika huko Mispa, wakateka maji na kuyamimina mbele za Bwana; wakafunga siku ile, wakasema huko, Tumemfanyia Bwana dhambi. Samweli akawaamua wana wa Israeli huko Mispa (1Samweli 7:6)**

Wana wa Israel walimtenda Mungu dhambi, na kuanza kufanya ibada kwa miungu ya baali, lakini walipomwomba Mungu kwa maombi ya kufunga walipata kibali na wakasamehewa dhambi zao.

**Yehoshafati akaogopa, akauelekeza uso wake, amtafute Bwana, akatangaza mbiu ya watu kufunga katika Yuda yote (2Nyakati 20:3).**

Baada ya mfalme kuona adui zake wameinuka juu yake na wameamua kupigana nae, aliamua kumwomba Mungu kwa maombi ya mzigo na kufunga na Mungu akaamua kumjibu na kumpa ushindi juu ya adui zake

## 4. SADAKA.

**Msijiwekee hazina duniani, nondo na kutu viharibupo, na wevi huvunja na kuiba. Bali jiwekeeni hazina mbinguni kusikoharibika kitu kwa nondo wala kutu wala wevi hawavunji wala hawaibi, kwa kuwa hazina yako ilipo, ndipo utakapokuwapo na moyo wako (Mathayo 6:19-21).**

Sadaka inaueleza moyo wa mtu mbele za Mungu, kwa hiyo unapotoa sadaka, Mungu anautazama moyo kuwa una kitu gani. Kupitia sadaka ni rahisi Mungu kujibu haja za moyo wako, kwa hiyo unapotoa sadaka ni muhimu ukaambatanisha na maombi na ndani ya moyo wako ukiwa umebeba imani ya kujibiwa.

**Palikuwa na mtu Kaisaria, jina lake kornelio akida wa kikosi kilichoitwa Kiitalia, mtu mtauwa mchaji wa Mungu, yeye na nyumba yake yote, naye alikuwa akiwapa watu sadaka nyingi na kumwomba Mungu daima. Akaona katika maono wazi wazi kama saa tisa za mchana, malaika wa Mungu akimjia na kumwambia, Kornelio akamtazama sana akaogopa akasema, kuna nini Bwana, akamwambia sala zako na sadaka zako zimefika juu na kuwa ukumbusho mbele za Mungu (Matendo ya Mitume 10:1-4).**

Katika mistari hii tunaona mfano wa Kornelio, alikuwa mmoja kati ya watu waliokuwa wanaombea sadaka walizokuwa wakitoa. Na biblia inatufundisha Mungu alipoziangalia zile sadaka na maombi yaliyoambatana na zile sadaka akaona ipo haja ya kumjibu. Kwa hiyo ni dhahiri kuelewa kuwa sadaka ndio ilibeba majibu ya maombi yake.

## 5. HEKIMA YA MATUMIZI YA NENO LA MUNGU.

Kuna baadhi ya maombi hayajibiwi kwa sababu tunaomba vibaya, hatuombi kwa ajili ya utukufu wa Mungu, ila tunaomba kwa ajili ya maslahi yetu wenyewe.

Biblia inasema kuwa:

**Hata mwaomba, wala hampati kwa sababu mwaomba vibaya, ili mvitumie kwa tamaa zenu (Yakobo 4:3).**

Shida sio kuomba tu, unaomba kwa ajili ya nini? Lengo la maombi ni nini? Kilichoweka msukumo wa kuomba ni nini? Ikiwa ni kwa ajili ya utukufu wa Mungu, Mungu hataacha kujibu lakini ikiwa unaomba kwa ajili ya tamaa binafsi ni vigumu Mungu kujibu hayo maombi.

## 6. BIDII KATIKA MAOMBI.

Bidii inaonyesha kiwango chako cha uhitaji wa jambo mbele za Mungu na pia inaonyesha uwezo wako wakukitunza kitu utakachopata, hii ni kwa sababu thamani ya kitu kwa mtu ipo katika gharama inayotumika kukipata.

**Kuomba kwake mwenye haki kwafaa sana, akiomba kwa bidii. Eliya alikuwa mwanadamu mwenye tabia moja na sisi, akaomba kwa bidii mvua isinyeshe, na mvua haikunyesha juu ya nchi muda wa miaka mitatu na miezi sita (Yakobo 5:16b-17).**

Biblia inamwelezea mtu ambaye ni mwenye haki na kwa hali ya kawaida hatukutegemea tuone neno kwa bidii kwa kuwa ni haki yake lakini anasema akiomba kwa bidii ndipo haki itakuja.

Watu wengi tunautumia mfano wa Eliya wa kufunga mvua isinyeshe kwa imani kabisa lakini tunaposoma mstari huu tunasahau kuna maneno yanasema **aliomba kwa bidii**, maana yake ingawa Eliya aliheshimiwa na Mungu katika njia zake lakini swala la yeye kupokea lilitegemea bidii ya maombi yake.

Baadhi ya mifano ya watu walioomba kwa bidii bila kukata tamaa ili wapokee majibu yao katika biblia:

Kanisa la mitume juu ya Petro

**Basi Petro akalindwa gerezani, nalo kanisa likamwomba Mungu kwa juhudi kwa ajili yake. Hata wakati Herode alipotaka kumtoa, usiku ule ule Petro alikuwa analala katikati ya askari wawili, amefungwa minyororo miwili; walinzi mbele ya mlango wakailinda gereza (Matendo ya mitume 12:5-6).**

Danieli juu ya taifa la Israeli

**Daniel 10:2, 12-13 Katika siku zile mimi, Danieli, nalikuwa nikiomboleza muda wa majuma matatu kamili.Ndipo akaniambia, Usiogope, Danieli; kwa maana tangu siku ile ya kwanza ulipotia moyo wako ufahamu, na kujinyenyekeza mbele za Mungu wako, maneno yako yalisikiwa; nami nimekuja kwa ajili ya maneno yako. Lakini mkuu wa ufalme wa Uajemi alinipinga siku ishirini na moja; bali, tazama, huyo Mikaeli, mmoja wa hao wakuu wa mbele, akaja kunisaidia; nami nikamwacha huko pamoja na wafalme wa Uajemi.**

Alijibiwa maombi toka siku ya kwanza lakini ajitia nia kwa Bwana kuahakikisha yanadhihirika mapka siku 21 na ndipo alipokea majibu ya maombi yake

Hana juu ya kupata mtoto

**1Samwel 1:10 Naye huyo mwanamke alikuwa na uchungu rohoni mwake, akamwomba Bwana akalia sana.**

## 7. MATUNDA YA KAZI.

Kuleta matokeo katika kazi uliyopewa na Mungu ni jambo la msingi sana na Mungu analiheshimu sana, na pia ni rahisi kuangalia matunda ya kazi yako na kujibu maombi yako

Bibilia inatuambia wazi kuwa:

**Si ninyi mlionichagua mimi, bali ni mimi niliyewachagua ninyi; nami nikawaweka mwende mkazae matunda; na matunda yenu yapate kukaa; ili kwamba lo lote mmwombalo Baba kwa jina langu awapeni (Yohana 15:16).**

Bwana Yesu anawaambia wanafunzi wake kuwa, mimi nimewaweka kwa ajili ya kunizalia matunda (kuongeza faida) ili mnapomwomba Baba kwa jina langu aweze kuwapa majibu ya maombi yenu. Hili ni jambo la msingi kwa Mungu,na mfano mzuri ni mfalme Hezekia.

**Siku hizo Hezekia akaugua, akawa katika hatari ya kufa. Isaya, nabii, mwana wa Amozi, akamjia akamwambia, Bwana asema hivi, Tengeza mambo ya nyumba yako; maana utakufa, wala hutapona. Basi Hezekia akajigeuza, akaelekeza uso wake ukutani, akamwomba Bwana akasema, Nakusihi, Bwana, ukumbuke sasa, jinsi nilivyokwenda mbele zako katika kweli na kwa moyo mkamilifu, na kutenda yaliyo mema machoni pako. Hezekia akalia sana sana. Ikawa, kabla Isaya hajatoka katika mji wa kati, neno la Bwana likamjia, kusema, Rudi, ukamwambie Hezekia, mkuu wa watu wangu, Bwana, Mungu wa Daudi baba yako asema hivi, Nimeyasikia maombi yako, na kuyaona machozi yako; tazama, nitakuponya; siku ya tatu utapanda nyumbani kwa Bwana. Tena, nitazizidisha siku zako, kiasi cha miaka kumi na mitano, nami nitakuokoa wewe, na mji huu, na mkono wa mfalme wa Ashuru, nami nitaulinda mji huu kwa ajili yangu, na kwa ajili ya Daudi, mtumishi wangu. (2Wafalme 20:1-6).**

Suala la kifo cha Hezekia lilikuwa limetoka kwa Mungu, na alimtuma nabii Isaya kumpelekea ujumbe huo, Hezekia aliposikia aliamua kumlilia Mungu kwa maneno mengine aliamua kumwomba Mungu na Mungu akamjibu sawasawa na maombi yake. Lakini kilichomsababisha Mungu kujibu hayo

maombi ni uaminfu na unyenyekevu aliokuwa nao Hezekia katika kazi yake na matunda ya kazi ndio maana aliongezewa miaka kumi na tano.

## 8. KUOMBA KATIKA MAPENZI YA MUNGU.

**Mapenzi ya Mungu** ni matakwa au makusudi ya Mungu. Ili maombi yapate kujibiwa ni lazima yaendane na mapenzi ya Mungu. Maisha ya mtu yameratibiwa na Mungu au kwa namna nyingine yapo katika mpango wa Mungu. Maana yake kitu ambacho kipo katika mpango wa Mungu unapokihitaji kwa njia ya maombi  ni rahisi Mungu kukujibu kwa kuwa kipo katika mpango wake.

**Na huu ndio ujasiri tulionao kwake, ya kuwa tukiomba kitu sawasawa na mapenzi yake atusikia, na kama tukijua kuwa atusikia tuombacho chochote, twajua kuwa tunazo zile haja tulizomwomba** (**1Yohana 5:14-15).**

Kwa kawaida mfumo wa maisha ya watu umefungwa katika utaratibu au maono na malengo. Ukipeleka pendekezo la uhitaji wa jambo lolote ambalo lipo kwenye utaratibu wa utendaji kazi ni rahisi sana kujibiwa tofauti na lile ambalo halipo kwenye mpango. Hii ndiyo sababu Biblia ikaandika kuwa tunakuwa na ujasiri, lakini hatuishii kuwa na ujasiri bali hata majibu ya maombi tumepokea.

**Akaenda tena mara ya pili, akaomba akisema, ikiwa haiwezekani kikombe hiki kiniepuke nisipokunywa mapenzi yako yatimizwe. Akaja tena akawakuta wamelala, maana macho yao yamekuwa mazito, akawaacha tena akaomba mara ya tatu, akisema maneno yaleyale (Mathayo 26:42-44).**

Ukifuatilia aina ya maombi aliyoyaomba Yesu mwanzo, yalikuwa ni ya kukataa kupita msalabani lakini mpango wa Mungu ulikuwa apite pale. Yesu kristo hakupata majibu mpaka alipobadili aina ya maombi na kuruhusu mapenzi ya Mungu yatimie, ndipo tunaona akipata amani ishara ya kupokea majibu.

## 8. NAFASI YA MTU MBELE ZA MUNGU.

Nafasi ni mahali sahihi mtu anapotakiwa kuwepo kwa wakati sahihi ili kukamilisha jambo lililokusudiwa. Nafasi imebeba haki ya mtu inayomwezesha maombi yake kujibiwa.

**Walinikabili siku ya msiba wangu; Lakini Bwana alikuwa tegemeo langu. Akanitoa akanipeleka panapo nafasi; Aliniponya kwa kuwa alipendezwa nami Bwana alinitendea sawasawa na haki yangu; Sawasawa na usafi wa mikono yangu akanilipa.** (**2Samweli 22:19-21)**

Mfalme Daudi alipokuwa katika wakati mgumu, macho yake alielekeza katika kumwomba Bwana, tunachokiona ni kwamba Mungu hakumwokoa moja kwa moja kwenye hali ngumu aliyokuwa nayo, bali alimhamisha na kumweka mahali anapotakiwa kuwepo yaani **mahali panapo nafasi,** kwa hiyo majibu ya maombi ya Daudi yasingeweza kuja kama asingehamishwa mahali pale alipo. Nafasi ndiyo iliyobeba majibu ya Daudi kuokolewa na ndiyo maana Mungu alimsaidia.

Nafasi ya mtu mbele za Mungu ina mchango mkubwa katika kumfanya huyo mtu kujibiwa au kutokujibiwa maombi yake. Katika hali ya kawaida ya maisha tunayoishi ili mtu akusaidie jambo fulani ni lazima awe anakufahamu vizuri. Kama hakufahamu vizuri anaweza asikusaidie kabisa au akakusaidia kidogo. Unapoomba Mungu anaangalia unaomba kama nani, au umesimama nafasi gani.

Zipo nafasi kadhaa mbele za Mungu ambazo hufanya maombi ya mtu kujibiwa au kutojibiwa.

## Nafasi ya kikuhani.

Kuhani ni mtu anayesimama au anayefanya maombi kwa ajili ya watu wengine, nafasi ya ukuhani humpa mtu haki ya kusimama mbele za Mungu na maombi yake kujibiwa kwa sababu tu ya ukuhani. Biblia inasema kuwa:

**Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi (Ufunuo wa Yohana 5:9-10).**

Katika Agano la Kale tunaelewa kuwa aliyekuwa na ruhusa ya kuomba kwa ajili yake na watu wake ni kuhani peke yake, lakini Biblia inasema alichinjwa akamnunua kila mtu na kumfanya au kumpa nafasi ya **ukuhan**i ikiwa na maana kuwa kazi alizokuwa akizifanya kuhani kwa sasa kila mtu ana nafasi ya kufanya kwa kuwa amefanyika kuhani. Kwa  hiyo kuna maombi ukiwa unafanya kwa ajili ya watu wengine ili Mungu akujibu anategemea ujiambatanishe na nafasi ya **kikuhani** kwa kuwa hiyo nafasi inakutambulisha mbele zake kuwa unastahili kupokea majibu ya watu.

## Nafasi ya kifalme.

**Mfalme** ni mtawala, ikiwa na maana mtu mwenye maamuzi ya mwisho na usemi wa mwisho katika eneo analoliongoza. Kauli ya mfalme imebeba amri, ushauri na suluhisho la jambo. Kuna maombi mengine ambayo unapofanya unatakiwa usimame kwenye nafasi hii ili kupokea majibu yake na ukiwa nje ya hii nafasi ni vigumu sana kupokea. Mfano Rais wa nchi sio kila muda atawaomba wananchi watekeleze majukumu yao bali kuna mtu atawaagiza wananchi kutekeleza, wakati mwananchi wa kawaida hana mamlaka ya kuagiza kitu kifanyike isipokuwa kuomba, sasa basi kuagiza na kuomba ni vitu viwili tofauti, kwa hiyo mtu aliyeokoka kuna muda katika maombi yake anatakiwa asimame kwenye nafasi ya kifalme kuamuru, au kuagiza vitu fulani vifanyike, lakini akiwa kama kuhani hawezi kuagiza isipokuwa kuomba.

**Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi. (ufunuo 5:9-10)**

Ametununua na kutufanya kuwa ufalme ikiwa na maana ya kutupa nafasi ya kiutawala na amri katika maombi yetu.

**Nafasi kama lango.**

**Inueni vichwa vyenu, enyi malango, Inukeni, enyi malango ya milele, Mfalme wa utukufu apate kuingia. (Zaburi 24:7)**

Lango linaweza kuwa mzaliwa wa kwanza katika familia, mtu wa kwanza kuokoka katika jamii, kiongozi wa kanisa, familia au ukoo, nk Kuna vitu Mungu hawezi kufanya kama hajaruhusiwa na mtu anayemtambua kama lango. Maana yake lango ndiye anayempa ruhusa ya kuingia kufanya yale yanayotakiwa na kama hautasimama katika nafasi ya lango ni vigumu sana kupokea majibu ya maombi yako kwa sababu Mungu anaangalia sauti ya aliyemweka katika nafasi hiyo.

# SURA YA TATU

# *UHUSIANO KATI YA KIZAZI CHAKO NA MAHUSIANO YAKO NA MUNGU*

Biblia imetupa nafasi ya kumjua Mungu pamoja  na faida zake, (**Ayubu 22:21 Mjue sana Mungu, ili uwe na amani; Ndivyo mema yatakavyokujia).**

Kumjua Mungu ni kuwa naye karibu katika maisha yako yaani kuwa na mahusiano mazuri naye. Na zaidi ya kuwa tunapata amani tunapomjua Mungu, na kwamba mema yanatujia, uhusiano wetu mzuri na Mungu unaweza kuleta faida kwa kizazi chetu kinachokuja.

Na uhusiano wa mtu na Mungu ukiwa mbaya unaathiri uzao wake na kusababisha kizazi chake pia kupita wakati mgumu.

Jambo kama hili liliwahi kuwatokea wana wa Israel,

**Baba zetu walitenda dhambi hata hawako; Na sisi tumeyachukua maovu yao. (Mambolezo 5:7)**

Taifa la Israel walikuwa kwenye wakati mgumu, wakatafuta chanzo cha magumu wanayopata, wakagundua kuwa chanzo ni baba zao. Maovu yaliyowatesa hayakuwa maovu yao, ila yalikuwa maovu ya baba zao. Walikuwa wanaona mama zao wamekuwa wajane, wao wenyewe walijiona kama yatima, na walikuwa wanauziwa kuni zao, wakajiuliza kwa nini haya yote yamewapata? Wakapata jibu kwamba ni kwa sababu ya maovu ya baba zao. Na hii ilitokea wakati baba zao walipomwacha Mungu au walipopoteza uhusiano wao na Mungu. Kwa hiyo ni muhimu sana kujenga mahusiano yako na Mungu ili kuhakikisha kizazi chako kinakuja kukaa vizuri. Biblia inasema baba zetu walitenda dhambi nao hawako.Maana yake nini? Dhambi

iliyotendwa na baba zao ndiyo inayoonekana kama alama inayowapa majuto mioyoni mwao.

**(Hosea 4:6) Kwa kuwa wewe umeyakataa maarifa, mimi nami nitakukataa wewe, usiwe kuhani kwangu mimi; kwa kuwa umeisahau sheria ya Mungu wako, mimi nami nitawasahau watoto wako.**

Mungu anasema.Mimi nami nitawasahau watoto wako, kilichomfanya Mungu aseme mimi nami nitawasahau watoto wako ni ile hali ya Israel kumkataa Yeye, watoto anaosema kuwa atawakataa hawajashiriki katika kumkataa Mungu, lakini Mungu anasema atawakataa. Jiulize kwa nini Mungu awakatae watoto ambao hawakuhusika? Ni kwa sababu wao walimkataa Mungu na kupoteza uhusiano wao na Mungu. Uhusiano wako na Mungu una nafasi kubwa sana katika kujenga kizazi chako na kuacha alama ambayo wataikumbuka kwa furaha wala sio kwa majuto, maana umewaandalia mazingira mazuri ya kumsikia Mungu.

**Mathayo 27:25 Watu wote wakajibu wakasema, Damu yake na iwe juu yetu, na juu ya watoto wetu.**

Hii ni habari za Yesu Kristo na Pilato kuhusu mashitaka waliyoleta wahayudi, Pilato alipoona huyu mtu hana hatia, na aliishi kwa haki hapa duniani, na habari wanazoeleza kuwa sio za kweli, akaamua kunawa mikono. Pilato aliamua kufanya tendo liliwaashiria wahayudi kuwa juu ya mtu (Yesu) mimi siendelei tena na alijua kuwa kila atakachofanya lazima aache alama, wahayudi wakajibu kile kitendo kwa maneno wakasema, **Damu yake iwe juu yetu, na watoto wetu.**

Jiulize vizuri, unazaliwa na unakua, inapofika wakati wa wewe kufanya maamuzi yako binafsi unashindwa kwa sababu kuna mtu ametangulia na ameshafanya mamuzi kwa niaba yako na maisha yako kwa ujumla.

Hata kama watoto wao wangekuja kukataa baadaye kuwa sisi hatuhusiki na hiyo damu, isingekuwa rahisi kwa sababu wazee wao walishaapa. Jambo la kushukuru ni kwamba walisamehewa ile dhambi pale pale msalabani.

Namna tunavyomjua Mungu na kuwa naye karibu tunatengeneza mazingira ya kizazi chetu (watoto wetu) kuwa na msingi mzuri wa maisha. Mahusiano yetu na Mungu hayaishii katika kumjua Yeye tu, bali katika kuyashika na kuyatenda mapenzi yake na kuzishika amri zake. Hii ndio maana aliwaambia wana wa Israel kuwa:

**Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, Bwana, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao,nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu (Kutoka 20:5).**

Mungu anamwambia Musa matokea ya kutumia hizi sheria (kutii au kupuuza) hayatakuwa kwao peke yao, bali kwa watoto wao pia, na sio hao tu hata watoto wa watoto wao, hadi kizazi channe. Kama watazishika sheria za Mungu maelfu elfu ya watu watapata rehema kutoka kwa Mungu. Neno maelfu elfu ni hesabu kubwa zaidi ya vizazi vinne alivyotaja kuviadhibu ikiwa tu hawatafuata sheria zake. Lengo la sheria hizi ni kuimarisha uhusiano wao na Mungu baada ya kuona kuwa wanaanza kumwacha Yeye na kumsahau. Kwa maana angeweza kumpa Adamu pale Edeni lakini hazikuhitajika kwa kipindi kile. Uhusiano wetu na Mungu unapoondoka, ule ukaribu wetu na Mungu nao huondoka. Ukaribu wetu na Mungu ukiondoka,tunashindwa kupokea vile vitu alivyokusudia kwa ajili yetu na kuachilia adhabu, na adhabu hii inaachiliwa kwetu na kwa vizazi vyetu.

Kwa maneno mengine, kile wanachokivuna watoto, (mabaya na mazuri) ni matokeo ya kilichofanywa na wazazi. Kama wazazi walifanya mabaya, maana yake walipanda mbegu mbaya, na kwa sababu ni mbegu lazima iote, inapoota haiwezi kuota na matokeo mazuri ikiwa wazazi walipanda mbegu mbaya.

Ikiwa wazazi wana uhusiano mzuri na Mungu watapanda mbegu nzuri itakayokuwa na matokeo mazuri kwa kizazi chao.

**Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha, na kuomba, na kunitafuta uso, na kuziacha njia zao mbaya; basi, nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao, na kuiponya nchi yao. Sasa macho yangu yatafumbuka, na masikio yangu yatasikiliza maombi ya watu waombao mahali hapa (2Mambo ya Nyakati 7:14-15).**

Ukianza kuusoma huu mstari, cha kwanza utakachoona ni toba, lakini tuangalie kwa sura nyingine kidogo. Mfalme Sulemani alimjengea Mungu hekalu, akafanya kwa jinsi alivyopewa maelekezo. Alipomaliza ujenzi wa hekalu na kabla hekalu halijaanza kutumika kwa ajili ya ibada, Sulemani alihakikisha anaweka alama ya kudumu ambayo ilitumika wakati wa uongozi wake, uongozi wa wafalme waliofuata baada yake na katika kizazi chetu leo hii. Alama aliyoweka Sulemani ni kuhakikisha kuwa kizazi kinachofuata kinaishi kwenye uwepo wa Mungu na hata itatokea wakamkosea Mungu. (**2Mambo ya Nyakati 6:34 Wakikukosa, (maana hakuna mtu asiyekosa),** aweze kuwa samehe. Sulemani alijua hilo ya kuwa hakuna mtu asiyemkosea Mungu, na kwa kujua hiloalikuwa amewafanyia maombi kwa Mungu.

Hayo maombi ya Sulemani ndio alama ninayozungumzia, ni maombi ya msingi sana yaliyolibeba taifa la Israel kwa muda mrefu na lilikuwa agano la Mungu kwa Sulemani.

**2Mambo ya nyakati 6:24-39 Ikiwa watu wako Israeli wamepigwa mbele ya adui zao, kwa sababu wamekukosa wewe; kama wakirejea kwako, na kulikiri jina lako, wakikuomba na kukusihi nyumbani humu; basi usikie huko mbinguni, ukaisamehe dhambi ya watu wako Israeli, na kuwarejeza tena katika nchi uliyowapa wao na baba zao. Ikiwa mbingu zimefungwa,**

hata hakuna mvua, kwa sababu wamekukosa wewe; kama wakiomba wakikabili mahali hapa, na kulikiri jina lako, na kuiacha dhambi yao, uwatesapo; basi usikie huko mbinguni, ukaisamehe dhambi ya watumwa wako, na ya watu wako Israeli; uwafundishapo njia njema iwapasayo waiendee; ukainyeshee mvua nchi yako, uliyowapa watu wako iwe urithi. Ikiwa nchi imeingia njaa, au tauni, au ukosefu wa mvua, au ukungu, au nzige, au panzi; ikiwa adui wamewahusuru katika nchi ya miji yao, au ukiwapo msiba wo wote, au uele wo wote; yo yote atakayoyaomba na kusihi mtu awaye yote, au watu wako Israeli wote pamoja, watakaojua kila mtu pigo lake mwenyewe, na msiba wake mwenyewe, akiinyoshea mikono nyumba hii; basi usikie huko mbinguni, ukaapo, ukasamehe, ukampatilize kila mtu kwa kadiri ya njia zake zote; wewe umjuaye moyo; (maana wewe peke yako ndiwe uijuaye mioyo ya wanadamu); ili wakuche wewe, waziendee njia zako, siku zote watakazoishi katika nchi uliyowapa baba zetu. Hata na mgeni naye, asiyekuwa mmoja wa watu wako Israeli, atakapokuja kutoka nchi iliyo mbali sana kwa ajili ya jina lako kuu, na mkono wako ulio hodari, na mkono wako ulionyoshwa; hao watakapokuja na kuomba wakiielekea nyumba hii; basi usikie huko mbinguni, toka makaoni mwako, ukatende yote atakayokuomba huyo mgeni; ili watu wote wa dunia wapate kulijua jina lako, na kukucha wewe, kama watu wako Israeli, tena wajue ya kuwa nyumba hii niliyoijenga imeitwa kwa jina lako. Ikiwa watu wako wametoka kupigana na adui zao, utakakowatuma ko kote, wakikuomba kuuelekea mji huu uliouchagua, na nyumba hii niliyoijenga kwa jina lako; basi uyasikie huko mbinguni wayaombayo, na kusihi, ukaitetee haki yao. Wakikukosa, (maana hakuna mtu asiyekosa), hata uwakasirikie, na kuwatia mikononi mwa adui zao, wawahamishe, na kuwachukua mateka mpaka nchi iliyo mbali au iliyo karibu; basi wakikumbuka katika nchi walikohamishwa, na kutubu, na kukusihi katika nchi ya uhamisho wao, wakisema, Tumekosa, tumetenda kwa ukaidi, tumefanya maovu; wakurudiapo kwa mioyo yao yote, na kwa nia zao zote, katika nchi ya uhamisho wao, adui walikowahamisha, wakiomba na kuielekea nchi uliyowapa baba zao, na mji huu

**uliouchagua, na nyumba hii niliyoijenga kwa jina lako; basi uyasikie toka mbinguni, toka makaoni mwako, wayaombayo, na kusihi, ukaitetee haki yao; ukawasamehe watu wako, waliokosa juu yako.**

Haya ni maombi ya mfalme Sulemani baada ya kujenga lile hekalu, na tumeona umuhimu wa alama aliyoweka, na hii ni kutokana na ukaribu wake yeye na Mungu. Ni muhimu sana kuwa na uhusiano mzuri na Mungu ili kuhakikisha wanaokuja nyuma yako, (kizazi chako) hakipati wakati mgumu kwa ajili yako uliyewatangulia.

Tazama habari za Yusufu, Mungu alikusudia mambo makubwa ndani yake, kikuu ilikuwa hatima ya miaka 14 ya nchi ya Misri. Kilichomsaidia kufanikisha hilo ilikuwa ni uhusiano mzuri aliokuwa nao na Mungu wake.

**Neno hilo likawa jema machoni pa Farao, na machoni pa watumwa wake wote. Farao akawaambia watumwa wake, Tupate wapi mtu kama huyu, mwenye roho ya Mungu ndani yake? (Mwanzo 41:37-38).**

Farao alitambua kuwa huyu mtu ni mtumishi wa Mungu (mwenye mahusiano mazuri na Mungu), na Roho wa Mungu anakaa ndani yake maana amefanyika baraka (mafanikio) kwa ajili ya nchi ya Misri na akaamua kumpa nafasi za utawala katika nchi yake.

Ukianzia **Mwanzo 41:25** Biblia inasema:

**Yusufu akamwambia Farao, Ndoto ya Farao ni moja; Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu. Wale ng'ombe saba wema ni miaka saba; na yale masuke saba mema ni miaka saba. Ndoto ni moja. Na wale ng'ombe saba, dhaifu, wabaya, waliopanda baada yao, ni miaka saba; na yale masuke saba matupu yaliyokaushwa na upepo wa mashariki, yatakuwa miaka saba ya njaa. Ndivyo nilivyomwambia Farao, ya kwamba Mungu amemwonyesha Farao atakayoyafanya hivi karibu.**

**Tazama, miaka saba ya shibe inakuja, katika nchi yote ya Misri. Kisha kutakuja miaka saba ya njaa baada yake; na shibe ile yote itasahauliwa katika nchi ya Misri, na njaa itaiharibu nchi. Wala shibe ile haitajulikana katika nchi kwa sababu ya njaa inayokuja baadaye, maana itakuwa nzito sana.**

Huu ni msaada mkubwa sana ndani ya nchi ya Misri na kwa uongozi wa Farao, maana ulihakikisha jamii ya watu wanapata chakula cha kuwatosha wakati wa njaa, na aliyekuwa sababu ya kufanikiwa kwa kiwango hiki ni Yusufu.

Tunachojifunza katika mafanikio haya ya Yusufu ni ule uhusiano wake mzuri na Mungu.

Jambo lingine ni kwamba unapoharibu mahusiano yako na Mungu unatengeneza msingi mbovu ambao ni vigumu kwa kizazi chako kuja kuutengeneza, kwa sababu hawajui chanzo ni nini.

**Angalia, siku zinakuja, nitakapoukata mkono wako, na mkono wa mbari ya baba yako, hata nyumbani mwako hatakuwako mzee. Nawe utalitazama teso la maskani yangu, katika utajiri wote watakaopewa Israeli; wala nyumbani mwako hatakuwako mzee milele(1Samweli 2:31).**

Hii ni habari ya wana wa Eli walipomkosea Mungu na akaamua kuwaua, pamoja na kwamba wale watoto walikufa, Mungu aliachilia adhabu nyingine kwa ukoo mzima na kizazi chao. Hili ni jambo la kusikitisha kidogo kwa sababu ukoo mzima ulikosa nafasi ya kupata hekima za wazee na nafasi ya kushauriwa. Kati ya koo zote zilizoko ndani ya kabila 12 za taifa la Israel, ukoo wao tu ndio hauna wazee.

Jambo la kujenga mahusiano na Mungu na kuweka mazingira mazuri kwa ajili ya watoto wake au kizazi chake alilifanya pia Mfalme Yehu mwana wa Yehoshafati baada ya kupakwa mafuta na kukaa kwenye kiti cha kifalme alianza kufanya kama Mungu alivyomwambia kupitia mtumishi wake Elisha.

Huu ni mpango wa Mungu wa kuondoa ibada za miungu ya baali katika Israel, na alimpa maelekezo haya mtumishi wake Eliya

**Na itakuwa atakayeokoka na upanga wa Hazaeli, Yehu atamwua; na atakayeokoka na upanga wa Yehu, Elisha atamwua (1Wafalme 19:17).**

Yehu baada ya kutambua hilo kuwa kuna jambo Mungu alikusudia kulifanya katika utawala wake aliamua kuingia katika utekelezaji wake. Alianza kwa kutuma ujumbe kuwa watoto wa mfalme Ahabu wauawe (**2Wafalme 10:7-30)**

**Ikawa, barua ilipowawasilia, waliwatwaa hao wana wa mfalme, wakawaua, watu sabini, wakatia vichwa vyao katika makapu, wakampelekea huko Yezreeli (2Wafalme 10:7).**

**Hivyo Yehu akawapiga wote waliosalia wa nyumba ya Ahabu katika Yezreeli, na hao wakuu wake wote, na rafiki zake, na makuhani wake, hata hakumwachia aliyesalia hata mmoja (2Wafalme 10:11).**

**Akasema, Wakamateni wa hai. Wakawakamata wa hai, wakawaua penye birika ya nyumba ya kukatia manyoya kondoo, watu arobaini na wawili; wala hakumsaza mtu wao awaye yote (2Wafalme 10:14).**

**Naye alipofika Samaria, aliwapiga wote waliomsalia Ahabu katika Samaria, hata akamwangamiza, sawasawa na neno la Bwana alilomwambia Eliya (2Wafalme 10:17).**

**Ikawa mara alipokwisha kutoa sadaka ya kuteketezwa, Yehu akawaambia walinzi na maakida, Ingieni mwapige; mtu awaye yote asitoke. Basi wakawapiga kwa makali ya upanga; walinzi na maakida wakawatupa nje, wakaenda mpaka mji wa nyumba ya Baali (2Wafalme 10:25).**

**Bwana akamwambia Yehu, Kwa kuwa umetenda vema kwa kufanya vilivyo haki machoni pangu, kuitendea nyumba ya Ahabu sawasawa na**

**yote yaliyomo moyoni mwangu, wana wako wa kizazi cha nne watakaa kitini mwa Israeli (2Wafalme 10:30).**

Mfalme Yehu alikuwa na mahusiano mazuri na Mungu na ndio kilichomsaidia kuhakikisha anaifanya ile kazi kwa uaminifu. Baada ya kukamilika kwa kazi ndio Mungu anamwambia kuwa jambo ulilofanya ni nzuri sana, kwa maana umetenda kama nilivyokusudia, na sasa uzao wako hadi kizazi cha nne watafurahia matunda  ya kazi yako. Jiulize mfalme Yehu angepuuza yale  na kufanya kinyume na maagizo ya Mungu kingetokea kitu gani? Badala ya baraka ingekuwa laana au adhabu na watoto wake wangejikuta wanateseka kwa ajili ya kosa la baba yao.

Kuna gharama kubwa sana inayowapata watu wa kizazi chako unapokuwa kwenye nafasi na kuharibu uhusiano wako na Mungu. Inaweza kuwachukua muda mrefu au kuwakosesha baraka za Mungu na kuwaletea laana. Mfalme Yeroboamu mwana wa Nebati alijenga madhabahu huko Betheli na Dani ili watu wapate kumwabudu.

**Kwa hiyo mfalme akafanya shauri, akafanyiza ng'ombe wawili wa dhahabu, akawaambia watu, Ni vigumu kwenu kupanda kwenda Yerusalemu; tazama, hii ndiyo miungu yenu, enyi Israeli, iliyowapandisha kutoka nchi ya Misri. Akamweka mmoja katika Betheli, na wa pili akamweka katika Dani. Jambo hili likawa dhambi, maana watu walikwenda kuabudu mbele ya kila mmoja, hata huko Dani. Tena akafanya nyumba za mahali pa juu, akafanya na watu wo wote, watu wasio wa wana wa Lawi, kuwa makuhani.(1Wafalme 12:29-31)**

# SURA YA NNE

## *FAHAMU MKAKATI ALIONAO MUNGU JUU YA MAISHA YAKO*

Mungu anahusika na anawajibika katika maisha yetu kwa asilimia mia mmoja, kwa sababu alituumba na kutuleta kwa ajili ya kazi yake (Kusudi). Ili tuweze kutimiza kusudi lake na kila kusudi aliloweka ndani yetu huleta utukufu kwa kwake. Serikali au shirika linapowaajiri watu linahusika katika namna ya kuwatunza na kuhakikisha wanakaa mazingira salama ili kuhakikisha utendaji wa kazi unaenda vizuri na kuleta ufanisi zaidi kazini. Lengo la serikali si tu waajiriwa wake wafaidike na ajira hiyo lakini pia mipango na mikakati yake ifanikiwe kwa kiwango kikubwa. Mungu alipotuumba na kutuweka duniani alituleta kwa ajili ya kutimiza kusudi lake (kwa maana hakuna hata mmoja aliyekuja kwa bahati mbaya duniani) na kusudi la Mungu linampa Yeye utukufu, ndio maana nasema Mungu anawajibika katika hilo.

Duniani hatujaja kutalii, Mungu ametupa dunia ili tuishi kwa utaratibu wake, pamoja na kwamba tunatakiwa tuitawale, hajatupa tuitawale kwa utaratibu wetu bali kwa utaratibu wake.

**Mungu akasema, Na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi (Mwanzo 1:26)**

Neno **kutawala** maana yake ni kuwa na mamlaka au madaraka juu ya nchi au vitu au watu. Kwa hiyo Mungu aliposema wakatawale alimaanisha wakawe na**mamlaka** na **madaraka** juu ya vitu vyote vilivyoko juu ya nchi. Mtawala ni mfalme, na neno la mfame ni sheria kwa hiyo Mungu ametupa nafasi ya kuwa waamuzi au wasemaji wa mwisho yaani kutamka neno litakalofanyika sheria.

Biblia inasema kuwa:

**Maana Bwana, aliyeziumba mbingu, asema hivi; Yeye ni Mungu; ndiye aliyeiumba dunia na kuifanya; ndiye aliyeifanya imara; hakuiumba ukiwa, aliiumba ili ikaliwe na watu. Mimi ni Bwana, wala hapana mwingine (Isaya 45:18)**

Mungu hakuumba dunia iwe tupu, aliumba tukae sisi wanadamu, ni mahali pekee alipochagua Mungu aweke maisha ya mwanadamu wala sio sayari nyingine. Na Mungu alipoumba mbingu na nchi alikuwa na malengo hayo kwamba mbinguni akae Yeye, duniani tukae sisi.

**Mbingu ni mbingu za Bwana, Bali nchi amewapa wanadamu (Zaburi 115:16).**

Hiyo mistari inatuonesha wazi kuwa mbingu ni za Mungu lakini nchi ametupa sisi wanadamu. Kwa maana hiyo mbingu ameziumba kwa ajili yake na dunia ametupa tuikae sisi na tuitawale.

Unaweza ukasema kuwa hiyo ni Agano la Kale, Biblia katika agano jipya inatuonesha wazi tunatawala juu ya nchi:

**Nao waimba wimbo mpya wakisema, Wastahili wewe kukitwaa hicho kitabu na kuzifungua muhuri zake; kwa kuwa ulichinjwa, ukamnunulia Mungu kwa damu yako watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa, Ukawafanya kuwa ufalme na makuhani kwa Mungu wetu; nao wanamiliki juu ya nchi (Ufunuo wa Yohana 5:9-10).**

Watu wengi wanafikiri kuwa mkakati anaoufanya Mungu kuwa wamiliki na watawala ni kwa ajili ya watu fulani maalum, au eneo fulani maalum au kikundi fulani maalum, hapana mkakati huu ni kwa watu wote. Ndio maana ya kusema **watu wa kila kabila na lugha na jamaa na taifa.**

Utakubaliana na mimi kuwa ufalme huwa unahama kutoka kizazi hadi kizazi, na mtoto wa mfalme ndiye anayekuja kuwa mfalme (mtawala). Na ili mtoto awe mfalme (aanze kutawala) ni lazima baba yake awe amefariki. Sisi ni watoto wa Mungu, na Mungu wetu (Baba yetu) hawezi kufariki, anaishi milele lakini katika hali hiyo hiyo ya kuishi milele anataka sisi tuwe wafalme (watawala). Hii ndio sababu ya kusema Mungu ni mfalme wa wafalme, sio mfalme wa watumishi! Maana yake, sisi ni wafalme lakini sio wafalme wakuu, na tunatawala chini ya mfalme mkuu (Mungu).

Tunaweza kuwa na mahusiano mazuri na watu wengine au vitu vingine ikiwa mahusiano yetu na Mungu yako vizuri. Na maamuzi tunayofanya bila Mungu yanaweza kuleta matokeo ambayo yanaweza yakamzuia Mungu kuingilia katikwa sababu hakuhusika na hayo maamuzi tangu mwanzo. Mungu alimwambia Ibrahimu, msikilize Sara mkeo kwa habari ya Ismael, maana tangu mwanzo ulimsikia yeye. Kupatikana kwa Ismael haukuwa mpango wa Mungu kwa Ibrahimu, na wakati Ismael anapatikana Mungu hakushirikishwa, ndio maana akamwambia msikilize mkeo Sara.

Dunia hii iliumbwa iwe mwendelezo wa ufalme wa mbinguni kwa sababu Mungu ni Roho kulingana (**Yohana 4:24)** kwa hiyo utawala wake pia sio katika ulimwengu wa mwili bali katika ulimwengu wa roho.

Kila mtu anapozaliwa, anazaliwa kwa lengo maalumu la kuja kutimiza kusudi la Mungu,na kusudi la kwanza ni la utawala. kwa hiyo mkakati wa Mungu kumleta mtu duniani ni kwa ajili ya kuja kutawala. Biblia inatuambia kuwa:

**Mtu ni kitu gani hata umkumbuke, Na binadamu hata umwangalie? Umemfanya mdogo punde kuliko Mungu; Umemvika taji ya utukufu na heshima; Umemtawaza juu ya kazi za mikono yako; Umevitia vitu vyote chini ya miguu yake (Zaburi 8:4-7).**

Neno umemtawaza ndilo neno linalotumika katika kuwasimika viongozi au wafalme yaani **watawala,** kwa hiyo mwanadamu alipowekwa duniani

hakuwekwa aishi hivi hivi, lakini aliwekwa ili atawale au kuongoza kazi zote ambazo Bwana Mungu alizopa kuzifanya.

Mungu aliiumba dunia na kumpa mwanadamu aitawale kwa niaba yake, kwa maneno mengine tungesema kila mwanadamu (mwnaume na mwamamke amepewa mamlaka ya kifalme ya kutawala dunia kwa niaba ya Mungu kufuata utaratibu wa mbinguni au utaratibu wa ufalme wa mbinguni.

Mungu alipomuumba mwanadamu na kuweka **sura yake** ndani ya huyo mwanadamu, alitaka mtu awe mwakilishi wake hapa duniani, yaani alitaka kujulikana kupitia mtu. Kwa hiyo upo duniani kwa ajili ya kazi maalum ya kumwakilisha Mungu popote ulipo, lakini sio Mungu peke yake tu, unawakilisha pamoja na ufalme wake kwa ujumla ambao amekupa dhamana ya kuusimamia hapa duniani.

# HITIMISHO.

Dunia inakadiriwa kuwa na watu billion 7.7 (wikipedia 2019) na kila mmoja amekuja ana kusudi lake analotakiwa kutimiza. Ikiwa tutakaa katika mpango wa Mungu na kufanya yale aliyokusudia kwa ajili yetu, ni dhahiri kabisa dunia ingekuwa mahali pa raha sana. Kwa sababu kila kinachohitajika duniani kingekuwa kinapatikana, leo hii kuna madaktari wanafanya uhandishi, kunawalimu wanafanya uuguzi, kuna wanasheria wamekuwa wana siasa, kinachoumiza zaidi kuna watu wenye wito wa Mungu wameacha huo wito na wameenda kufanya kazi nyingine nje ya mpango wa Mungu. Matokeo yake ni kwamba wanapofanya kazi zao wanahisi ugumu sana na hawana amani kabisa ndiyo maana tunahisi kupungukiwa.

Hatuwezi kuijaza dunia na kuifanya kuwa sehemu salama kwa kila mmoja wetu, ikiwa kila mtu akijiangalia na kufikiri mambo yake mwenyewe. Leo hii tunanufaika na matunda ya watu  wengine waliomua kujitoa kwa ajili ya kuhakikisha wanaacha alama au kumbukumbu kwa ajili ya wengine na huenda leo unafurahia mambo yaliyofanywa na wengine. Pengine walioamua kugundua hivo vitu hawapo tena duniani lakini walifikiri kwa ajili ya wengine, basi nasi tunakaribishwa kuwafikiria na wengine ili waweze kufurahia matunda ya kazi zetu.

**MUNGU AKUBARIKI SANA NINAKUPENDA KATIKA KRISTO YESU.**

# VITABU REJEA.


**Mikakati Saba Ya Kujenga Ufalme Wa Mungu Kwa Njia Ya Maombi-*Mwl Christopher Mwakasege.***

**Praying To Get Result- *Kenneth Hagin.***


**Vitu Vya Msingi Katika Kujenga Mahusiano Yako Na Mungu Kwa Njia Ya Maombi- *Wilibath Thomas.***

**Purpose Of Driven Life On Earth- *Rick Warre.***

UNAWEZA KUJIPATIA KITABU KINGINE KILICHOANDIKWA NA MWALIMU HERIEL MICHAEL KIITWACHO ***IMANI ITENDAYO KAZ NDANI YETU.*** PIGA SIMU NAMBA+255 746 155 205

PIA JIANDAE KUPOKEA VITABU VIPYA VINAVYOFUATA

1. **NGUVU YA MAOMBI YA KUFUNGA**
2. **NI ZAMU YAKO SASA**


Heriel Michael ni mwalimu wa neno la Mungu, Amesoma shule ya msingi Endanachan 2001-2007, na shule ya sekondari ya Philip Marmo 2008_2011 na amewahi kuwa mwenyekiti UKWATA 2009-2010 Na Mwenyekiti wa madhehebu yote ya dini (MUUNGANO) 2009-2010 akiwa shule ya sekondari. Amesoma kidato cha tano na sita shule ya sekondari Mkuu Rombo.
Kwa sasa anasoma shahada ya kwanza ya uuguzi (Bachelor of Science in Nursing) katika chuo kikuu cha Dodoma na kwa neema ya Mungu ni mwenyekiti wa kamati ya uinjilisti kitivo cha Elimu. Kwa neema ya Mungu pia amepata kibali cha kutumika na kufanya huduma ndani na nje ya chuo kwa muda wote aliokuwa chuoni.
Email: herielmichael1@gmail.com
Cell: +255685148856/+255746155205
Mwandishi wa kitabu hiki chenye Jina IMANI ITENDAYO KAZI NDANI YETU anataka kuwakumbusha wakristo wote na wasomaji wa vitabu kuwa Imani ni kitu cha muhimu sana katika maisha ya Ukristo.
Ni matumaini yangu kuwa kupitia kitabu hiki Mungu atakusaidia ili kupitia Imani yako uliyonayo akupe neema na Baraka katika kumtumikia Yeye na kumpenda Zaidi.
TRUTH
IMANI
Itendayo Kazi Ndani Yetu
HERIEL MICHAEL